KAULI ZA NASAHA KATIKA HARUSI ZINAVYOJENGA UHUSIANO WA WANANDOA: Mifano kutoka Harusi za Wapemba

FATMA YAKOUT BIROLI

SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR

SUZA

DISEMBA, 2021

KAULI ZA NASAHA KATIKA HARUSI ZINAVYOJENGA UHUSIANO WA WANANDOA: Mifano Kutoka Harusi za Wapemba

Na

FATMA YAKOUT BIROLI

MA.K/3/2018/01/TZ

TASNIFU INAYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA KUKAMILISHA MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI KATIKA CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR (SUZA)

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR

SUZA

DISEMBA, 2021

ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma tasnifu hii yenye mada **Kauli za Nasaha katika Harusi Zinavyojenga Uhusiano wa Wanandoa: Mifano kutoka harusi za Wapemba** na anapendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kwa ajili ya kukamilisha sehemu ya masharti ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

……..…… **……**

DKT. OMAR SALUM MOHAMED **TAREHE**

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA TAIFA CHA ZANZIBAR

TAMKO NA HAKIMILIKI

TAMKO

Mimi **Fatma Yakout Biroli** ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika chuo kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada kama hii au shahada nyengine yoyote.

…….

Saini

……

Tarehe

HAKIMILIKI

Tasnifu hii inalindwa na sheria za hakimiliki za kitaifa na kimataifa. Hairuhusiwi kwa namna yoyote ile kunakili kazi yote au sehemu ya kazi hii bila ya idhini ya maandishi ya mwandishi au Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar isipokuwa kutumia sehemu ndogo kwa lengo la utafiti au kujisomea au kufanya uchambuzi yakinifu wa kitaaluma.

SHUKURANI

Shukurani za pekee ni zake Allah (S.W) kwa kunijaalia afya njema, nguvu pamoja na maarifa mazuri katika kipindi chote cha kutayarisha kazi hii. Kisha sala na salamu zimwendee kipenzi chetu Mtume Muhammad (SAW) mbora wa Mitume.

Shukurani zangu za dhati zimwendee msimamizi wangu Dkt. Omar Salum Mohamed kwa mashirikiano mema katika kunielekeza na kuniongoza bila ya kuchoka. Nathubutu kusema kuwa kama si mchango wake mkubwa alioutoa katika kazi hii isingaliweza kukamilika na kufikia kiwango hiki leo.

Nawashukuru wahadhiri wote walionifundisha na walionishauri katika kipindi chote cha masomo yangu. Pia shukurani zangu za dhati ziwaendee Mkuu wa Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Dkt. Asha Mhene Hamad na Mkuu wa Idara ya Kiswahili Dkt. Masoud N. Mohammed kwa kuwa nasi bega kwa bega katika kipindi chote cha mchakato wa masomo paamoja na utafiti kwa kutushajiisha, kutuelekeza na kutushauri ili kufikia ufanisi ulio bora.

Halikadhalika nawashukuru wanafunzi wenzangu wa shahada ya uzamili wa mwaka 2018 na uzamivu wa mwaka 2017 na 2018 kwa kushirikiana, kushauriana na kusaidiana katika harakati mbalimbali katika masomo yetu tukiwa darasani na hata nje. Pia shukurani zangu za dhati kwa Bi Kauthar A. Suleiman, Bi Mwamvita O. Chande na Bi Halima A. Hassan kwa mashirikiano yao pamoja na mchango wao mkubwa wa hali na mali walioutoa katika masomo yangu.

Shukrani hizi hazitakamilika kama sitamshukuru mume wangu mpenzi kwa msaada wake mkubwa wa hali na mali pamoja na uvumilivu wake wa hali ya juu katika

kipindi chote cha masomo yangu. Jambo hili lilinipa faraja kubwa na kunifanya nisome kwa utulivu bila ya kuwa na wasi wasi wowote moyoni mwangu.

Mwisho napenda kuwashukuru wale wote walioshiriki kutoa taarifa za utafiti huu na wale waliosaidia kwa njia moja au nyengine katika kufanikisha kazi hii. Niseme ahsanteni kwa masharikiano mema niliyoyapata kutoka kwenu.

TABARUKU

Kazi hii naitabaruku kwa wazazi wangu wapenzi bwana Yakout Biroli Yakout na bibi Siti Muadhin Juma kwa kunilea, kunifundisha maadili mema na kuniendeleza kielimu mpaka kufikia kiwango hiki, Allah awape khatima njema, awabariki na awalipe kila la kheri hapa duniani na siku ya hesabu.

VIFUPISHO

BAKITA	Baraza la Kiswahili la Taifa
BAKIZA	Baraza la Kiswahili la Zanzibar
TUKI	Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili

YALIYOMO

ITHIBATI YA MSIMAMIZI i

TAMKO NA HAKIMILIKI ii

TAMKO ii

HAKIMILIKI iii

SHUKURANI iv

TABARUKU vi

VIFUPISHO vii

IKISIRI xii

SURA YA KWANZA 1

UTANGULIZI 1

1.1 Usuli wa Mada 1

1.2 Tatizo la Utafiti 4

1.3 Malengo ya Utafiti 5

1.3.1 Lengo Kuu 5

1.3.2 Malengo Mahsusi 5

1.3.3 Maswali ya Utafiti 5

1.4 Umuhimu wa Utafiti 5

1.5 Mipaka ya Utafiti 6

1.6 Muhtasari wa Sura 6

SURA YA PILI 7

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA 7

2.1 Utangulizi 7

2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi 7

2.2.1 Kauli za Nasaha katika Nyimbo za Harusi 7

2.2.2 Kauli za Nasaha katika Mila na Desturi za Harusi 10

2.3 Pengo la Utafiti 11

2.4 Nadharia ya Uchambuzi Makini wa Matini (Critical Discourse Analysis) 12

2.5 Muhtasari wa Sura 15

SURA YA TATU 16

MBINU ZA UTAFITI 16

3.1 Utangulizi 16

3.2 Mkabala wa Utafiti 16

3.3 Eneo la Utafiti 16

3.4 Sampuli na Usampulishaji 17

3.4.1 Usampulishaji 17

3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa 17

3.5 Mbinu za Kukusanyia Data 18

3.5.1 Dodoso 18

3.5.2 Usaili 19

3.5.3 Ushuhudiaji 20

3.6 Vifaa vya Kukusanyia Data 20

3.7 Mbinu za Uchanganuzi wa Data 20

3.8 Uthibiti na Kuaminika kwa Data 21

3.9 Miiko ya Utafiti 21

3.10 Muhtasari wa Sura 22

SURA YA NNE 23

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA 23

4.1 Utangulizi 23

4.2. Uainishaji wa Kauli za Nasaha 23

4.2.1 Kauli za Nasaha za Biharusi 23

4.2.1.1Kauli za Nasaha katika Posa 24

4.2.1.2 Kauli za Nasaha katika Ndoa 31

4.2.2 Kauli za Nasaha za Bwanaharusi 42

4.2.2.1 Kauli za Nasaha katika Posa 43

4.2.2.2 Kauli za Nasaha katika Ndoa 47

4.3 Kauli za Nasaha Zinavyojenga Uhusiano wa Wanandoa 60

4.3.1 Wanandoa Huishi kwa Furaha katika Maisha ya Ndoa 61

4.3.2 Wanandoa Huleana katika Misingi Mema 61

4.3.3 Mume na Mke kuwa na Mashirikiano Mema 62

4.3.4 Wanandoa Hujengeana Heshima 62

4.3.5 Wanandoa Huishi kwa Kuhurumiana 63

4.3.6 Wanandoa Huepukana na Migogoro katika Ndoa 63

4.3.7 Wanandoa Huwa Wavumilivu katika Ndoa..... 64

4.3.8 Wanandoa Hupata Utulivu katika Ndoa 64

4.3.9 Wanandoa Huongezeka Kipato (Uchumi) 65

4.3.10 Mke na Mume Huishi kwa Kushauriana..... 65

4.3.11 Wanandoa Hupata Ukumbusho..... 66

4.3.12 Wanandoa Hubadilika Kimwenendo 66

4.3.13 Wanandoa kuwa na Ujasiri 67

4.3.14 Matayarisho ya Kuingia katika Ndoa..... 67

4.3.15 Wanandoa Hufahamu Wajibu Wao 68

4.4 Muhutasari wa Sura 69

SURA YA TANO 70

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO..... 70

5.1 Utangulizi 70

5.2 Muhtasari wa Utafiti 70

5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti 72

5.3.1 Kuainisha kauli za nasaha anazopewa biharusi na bwanaharusi kwa mujibu .. 72

5.3.2 Kufafanua uhusiano wa ndoa unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi. . 73

5.4 Hitimisho 73

5.5 Mapendekezo ya Utafiti 74

MAREJEO..... 75

VIAMBATANISHO 77

Kiambatanisho A: Maswali ya usaili kwa wanandoa wakongwe 77

Kiambatanisho B: Mwongozo wa maswali ya usaili kwa mashekhe 78

Kiambatanisho C: Mwongozo wa maswali ya dodoso kwa wanandoa wapya..... 79

Kiambatanisho D: Mwongozo wa maswali ya usaili kwa makungwi 80

Kiambatanisho E: Mwongozo wa maswali ya usaili kwa walimu wa kike 81

Kiambatanisho F: Ratiba na mchakato wa utafiti 82

Kiambatanisho G: Bajeti 83

Kiambatanisho H: Kibali cha utafiti 84

Kiambatanisho I: Ruhusa ya kufanya utafiti 85

IKISIRI

Utafiti huu ulikuwa na lengo la kuchunguza kauli za nasaha katika harusi za Wapemba jinsi zinavyojenga uhusiano wa wanandoa. Utafiti ulikuwa na malengo mawili: Kuainisha kauli za nasaha anazopewa biharusi na bwanaharusi kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wapemba na kufafanua uhusiano wa ndoa unaojengwa na kauli hizo. Utafiti uliongozwa na nadharia ya uchambuzi makini wa matini. Utafiti ulifanyika katika wilaya mbili, Chake chake na Mkoani. Data zilikusanywa kupitia mbinu ya dodoso, usaili na ushuhudiaji. Sampuli ya watafitiwa thelathini (30) ilitumika. Utafiti umebaini kuwa kauli za nasaha zitolewazo katika harusi za Wapemba. Ziko kauli za nasaha ambazo zimefanana na zinajenga uhusiano baina ya biharusi na bwanaharusi katika maisha ya ndoa. Mfano “Jihadhari sana, usimruhusu mke kuwa na marafiki wengi na kutumia muda mwingi nje kwa kukaa na marafiki zake.” “Tahadhari sana na ulimi, tunakunasihi, ulimi wako unatakiwa utumie vizuri.” Pia mtafiti amegundua kauli za nasaha zimefanikiwa kuonesha uhusiano unaojengwa na kauli hizo kwa bwanaharusi na biharusi. Mfano wa kauli za nasaha zinazojenga uhusiano kwa bwanaharusi na biharusi: “Tunakunasihi, mke ni mkeo, ndio mwenzio usimfanyie jeuri wala dharau.” “Zingatia vizuri tunayokunasihi, umuheshimu mumeo umuone ni mumeo wala usimdharau.” Mtafiti anapendekeza kuwa kauli za nasaha ziendelee kutumika katika jamii ya Wapemba na jamii nyengine za Waswahili. Pia mtafiti anapendekeza uchunguzi zaidi ufanyike katika uwanja wa kitaaluma utakaohusisha kauli za nasaha katika miktadha tafauti ikiwemo msibani, maofisini, mashuleni na miktadha mengineo ili kuzijenga jamii kuwa na maadili bora katika sehemu zote wanapokuwepo. Pia mtafiti anapendekeza watafiti wengine waangalie kauli za nasaha walizopewa wanandoa wakongwe na wanandoa wa sasa halafu walinganishe wepi waliofanikiwa kudumu katika ndoa zao.

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Usuli wa Mada

Neno nasaha limetolewa fasili na wataalamu kadhaa. Baraza la Kiswahili la Taifa [BAKITA] (2017) limeeleza kuwa nasaha ni maneno ya busara yenye kuasa yanayotolewa kwa watu kwa lengo la kuwaongoza maishani. Nalo Baraza la Kiswahili la Zanzibar [BAKIZA] (2010) limefafanua kuwa nasaha ni mawaidha au maelekezo anayopewa mtu ili kuufanya moyo wake uridhie jambo. Kutokana na fasili hizo, inabainika kwamba nasaha ni kauli ambazo hutolewa kwa ajili ya kumuelekeza mtu juu ya jambo fulani kwa lengo la kumsaidia.

Kuna kauli za nasaha ambazo hutolewa na wazazi. Hizi, lengo lake ni kuwajenga watoto kuwa na tabia njema. Mfano kuwaheshimu wakubwa, kuepuka ugomvi baina yao. Halikadhalika, kauli za nasaha hutolewa kwa wasichana wanapokuwa wari na wavulana wanapoingia baleghe. Katika jamii za jadi wari walipelekwa unyagoni kwa makundi. Huko walipewa kauli za nasaha na mafunzo mengine kuhusiana na maisha ya utu uzima. Lakini katika jamii za sasa mwari hupewa kauli za nasaha na somo yake.

Somo ni mtu maalumu anayeteuliwa na mama mzazi. Somo hukaa na mwari kwa siku kadhaa ili kumuelekeza mambo ya kumfanya ajitambue kwamba yumo katika hatua nyengine ya maisha. Hiyo huwa ni hatua ya mabadiliko ambapo mwari huyu huwepo katika kipindi kigumu cha ‘hatari’ (Mohamed, 2010). Katika kipindi hichi kama kauli za nasaha hazitolewi huenda utu wake ukafifia. Hata hivyo, mambo ya wari kuwekwa ndani yanatoweka kwa kasi kubwa katika zama hizi za utandawazi.

Pamoja na utandawazi uliosababisha wari wasiwekwe ndani lakini ilivyo hasa, kila hatua aipitayo msichana hupatiwa kauli za nasaha. Lengo ni kumjenga vyema kitabia ili daima awe ni kigezo kizuri kwa wengine. Hivyo basi, msichana huyu hufungamana na 'maisha ya kauli za nasaha' tangu siku anayovunja ungo. Kauli za nasaha huzidishiwa pale kikundi cha watu kinapofika nyumbani kwao kwa nia ya kupeleka posa.

Kwa upande mwengine, mabaleghe wa enzi za jadi walikuwa wakipelekwa jandoni. Huko walikuwa wakifunzwa mambo ya kiutu uzima pamoja na kufanyiwa jando. Hivyo, sherehe za kuingia kwenye baleghe ziliambatana na sherehe za kufanyiwa tohara. Hata hivyo kwa sasa mambo haya yametoweka. Wavulana hawaendi tena kama zamani wala hawawekwi ndani kwa ajili ya mafunzo. Hali ilivyo sasa ni kwamba wari na mabaleghe hupewa kauli za nasaha za utu uzima zaidi wakati wa harusi zao.

Harusi limefasiliwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili [TUKI] (1981), kuwa ni ndoa, nikahi, uozi, akdi. Pia TUKI (2010) harusi ni sherehe ya mke na mume ya kuoana kwa mujibu wa sharia. Kutokana na fasili hizi harusi ni tukio la kufunga mkataba kati ya mke na mume wa kuishi pamoja kama wanandoa. Kwa mujibu wa BAKIZA (2010) harusi ni sherehe ya ndoa halali.

Utafiti huu umetumia fasili zilizotolewa na BAKIZA (2010) pamoja na ile ya TUKI (1981) na TUKI (2010). Hii ni kwa sababu, kwa mujibu wa utafiti huu harusi inajumuisha mambo yote yanayofungamana na tendo la kufunga ndoa, ikiwemo posa, uradi, singo, ndoa na siku ya vyombo. Katika hatua zote hizo maharusi hupewa kauli za nasaha zinazohusiana na maisha ya ndoa.

Mbinu za kutolea kauli za nasaha za ndoa na maisha kwa ujumla zinabadilika kutokana na kubadilika kwa utamaduni. Jando na unyago kama mbinu za asili za kutolea kauli za nasaha zimeachwa na wakati. Hata hivyo, kauli za nasaha hazijasita kutolewa kila uchao. Kauli hizo ndizo ambazo hutawala hasa, kwenye harusi za Wapemba.

Katika harusi, kauli za nasaha hutolewa katika mazingira tofauti. Kuna kauli za nasaha ambazo hutolewa katika posa. Posa ni maombi ya kutaka kuoa yanayopelekwa na mtu kwa wazazi wa binti anaetarajiwa kuolewa (BAKIZA, 2010). Kwa mujibu wa mtandao wa https://www.jamiiforums.com posa ni kule kwenda kujitambulisha kwa binti kama unataka kuoa. Katika jamii ya Wapemba huwa na utaratibu maalumu wa kupeleka posa. Aghlabu huchaguliwa watu wawili mpaka watatu ambao ni watu wa makamo wanaoaminika wenye busara na heshima kwenda kuposa. Watu hawa hujulikana kama "washenga" ambao husimamia mchakato mzima wa posa hadi kuhakikisha kuwa ufungaji wa ndoa umekamilika. Pia litokeapo tatizo kwenye ndoa hiyo washenga ndio wahusika wa kutafuta suluhu.

Kuna kauli za nasaha pia zinazotolewa katika uradi. Hili ni tukio maalumu linalowakutanisha wanawake kwa nia ya kumuwaidhi biharusi mtarajiwa. Katika maandalizi ya uradi, familia ya harusi huwapa mwaliko baadhi ya watu kwa ajili ya kutoa kauli za nasaha kwa biharusi mtarajiwa ili ajengeke vyema katika maisha mapya ya ndoa.

Halikadhalika, katika harusi, kauli za nasaha huendelea kutolewa wakati ule singo linapofanyika. Hili ni tukio mahususi ambapo biharusi mtarajiwa husingwa mwilini kwa kunadhifishwa kutokana na maadini asilia ili ang'are na kumpendezesha

mumewe. Wakati wa kusingwa, biharusi hupewa kauli za nasaha zinazohusu mambo kadhaa ya kinyumba ambayo hupasa kutendeana baina ya mke na mume wanapokuwa pamoja ili kuimarisha ndoa yao.

Pia kauli za nasaha huendelea kutolewa siku ya ndoa yenyewe. Muda mchache kabla ya bwanaharusi kuja kumchukua biharusi (mke) wake, watu huingia ndani kumuona biharusi. Hapo humpongeza na kumpa kauli za nasaha.

Siku mbili au ya tatu baada ya ndoa kufungwa, jamaa wa pande mbili (bwanaharusi na biharusi) hukutana. Siku hii huitwa siku ya vyombo au kukabidhiana ulezi. Kama kawaida kauli za nasaha hutolewa katika mkusanyiko huo. Zaidi ya hayo, kauli za nasaha hupatikanwa kutoka kwa makungwi ambao huwapeleka maharusi nyumbani kwao na kukaa nao kwa kipindi kifupi; siku tatu hadi saba.

Haya yote yanaonesha kwamba Wapemba wanakitilia mkazo mkubwa kipengele cha kauli za nasaha. Jambo hili lilimfanya mtafiti aamue kuchunguza kwa kina kauli za nasaha wanazopewa maharusi katika kila hatua ya harusi ili kujua utamaduni huo unavyojenga uhusiano na mamlaka katika maisha ya ndoa.

1.2 Tatizo la Utafiti

Ingawa baadhi ya watafiti walizichunguza harusi za Wapemba katika hali anuwai, bado hapana mtafiti aliyezama katika mawanda yaliyobainisha kauli za nasaha za bwanaharusi na biharusi na namna kauli za nasaha zinavyojenga uhusiano baina ya bwanaharusi na biharusi katika maisha ya ndoa.

1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti uliongozwa na lengo kuu ambalo limefungamanishwa na malengo mahsusi kama yanavyoonekana hapa chini.

1.3.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la utafiti uliofanyika ni kuchunguza miktadha ya kauli za nasaha katika harusi za Wapemba.

1.3.2 Malengo Mahsusi

a) Kuainisha kauli za nasaha anazopewa biharusi na bwanaharusi kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wapemba.
b) Kufafanua uhusiano wa ndoa unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi.

1.3.3 Maswali ya Utafiti

a) Ni kauli gani za nasaha anazopewa biharusi na bwanaharusi kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wapemba?
b) Ni uhusiano gani unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi?

1.4 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una umuhimu ufuatao: Moja, itawaelimisha wanajamii kufahamu kauli za nasaha anazopewa biharusi na zile za bwanaharusi kwa mujibu wa utamaduni wa Wapemba. Vilevile jamii itaelewa uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha hizo. Pili, utafiti huu, utasaidia kuwachochea watafiti kufanya tafiti zao katika maeneo mengine ya jamii ambapo kauli za nasaha hutolewa kama msibani, mashuleni. Tatu,

utafiti huu unatarajiwa kuwa ni hazina mojawapo muhimu ya jamii katika ushawishi wa kujenga umoja na mashirikiano kutokana na kauli za nasaha zitolewazo kwenye harusi za Wapemba kama ni sehemu ya silka na utamaduni wao. Inatarajiwa pale jamii itakapoisoma kazi hii ndipo itaweza kuandaa mbinu bora za kuwapa kauli za nasaha wanandoa ili kuimarisha na kudumisha ndoa zao.

1.5 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulijikita katika miktadha ya nasaha katika harusi za Wapemba. Mambo yaliyoangaliwa ni kauli za nasaha anazopewa biharusi na bwanaharusi kutokana utamaduni wa Wapemba pamoja na uhusiano unaojengwa na kauli hizo kwa maharusi katika maisha yao ya ndoa. Hivyo, utafiti huu haukugusia kauli za nasaha katika miktadha mengine.

1.6 Muhtasari wa Sura

Sura hii imegusia miktadha inayotumika kutolea kauli za nasaha. Msisitizo mkubwa umejikita katika miktadha ya kauli za nasaha katika harusi. Miktadha hiyo itatoa njia ya kufikia lengo kuu la utafiti la kuchunguza uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha za harusi. Aidha ili kufikia lengo hili sura hii imebainisha malengo mahasusi yatakayoongoza utafiti huu. Sura hii vilevile imeeleza umuhimu wa kauli za nasaha, mfano kujenga maadili katika ndoa. Umuhimu huu na mengine yaliyoelezwa katika sura hii yamesaidia kuonesha umuhimu wa utafiti huu. Sura inayofuata inahusu mapitio ya kazi tangulizi pamoja na kiunzi cha nadharia kilichoongoza utafiti huu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA NADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii imeundwa na sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza ni mapitio ya kazi tangulizi na sehemu ya pili ni kiunzi cha nadharia.

2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Mapitio haya yalihusu kauli za nasaha katika nyimbo za harusi pamoja na mila na desturi za harusi

2.2.1 Kauli za Nasaha katika Nyimbo za Harusi

Said (2012), alichunguza maadili ya unyumba katika nyimbo za harusi. Alibainisha kuwa kupitia nyimbo hizo maharusi huelekezwa mambo kadhaa juu ya maadili ya unyumba. Nayo ni ustahamilivu wa shida au matatizo, kutunza siri, heshima kwa mume, kukaribisha wageni na kutokuwa na tabia mbaya zinazo kwenda kinyume na jamii. Kazi hii ilimpatia fununu mtafiti kwamba katika harusi za Waswahili kuna desturi ambayo wale wanaotarajiwa kufunga ndoa hupatiwa kauli za nasaha ili kuwajenga katika ndoa zao. Kazi ya Said iliangalia maadili ya unyumba katika nyimbo za harusi wakati utafiti huu uliangalia uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha katika harusi za Wapemba.

Timamy (2002), alishughulikia nyimbo za harusi katika sherehe mbalimbali za ndoa kuanzia wakati wa kuposwa kwa msichana hadi kufikia siku ya harusi kupitia baadhi ya jamii ya Waswahili wa Mombasa. Kazi hii ilitoa mwanga kwa mtafiti katika

kuelewa miktadha mbalimbali ya nyimbo zinazoimbwa harusini. Utafiti huo ulimsaidia mtafiti kugawa miktadha ya nasaha zinazotolewa na Wapemba katika harusi zao.

Nkwera (1998), alichunguza nyimbo za harusi kama kundi moja wapo la nyimbo za sherehe. Kulingana na Nkwera, alifafanua kuwa nyimbo nyingi za harusi zimejaa mambo ya mapenzi na ishara mbalimbali zinazowaelekeza maharusi kuhusu maisha yao pamoja na kupendana. Anafafanua zaidi kuwa kuna nyimbo ambazo huimbwa wakati wa kupokea mahari pamoja na siku ya kufunga ndoa. Kazi hii, ilisaidia kupata mwanga mtafiti katika kuchunguza kauli za nasaha katika harusi zinavyojenga uhusiano wa wanandoa wa Wapemba.

Ngure (2003), alieleza kuwa nyimbo za harusi huimbwa wakati wa furaha katika jamii nyingi nchini Kenya. Pia zipo nyimbo ambazo huimbwa kuelezea masikitiko ya kuondoka kwa binti alikokuzoea na kwenda asikokuzoea (asikokujua). Licha ya kuwa Ngure na mtafiti wa kazi hii wameangalia muktadha sawa wa harusini lakini Ngure aliangalia nyimbo za harusi wakati mtafiti wa kazi hii aliangalia kauli za nasaha katika harusi za Wapemba zinavyojenga uhusiano wa Wanandoa.

Mazigwa (1991), aliangalia nyimbo zinazoimbwa katika sherehe, mfano nyimbo zinazoimbwa katika sherehe za harusi, sherehe za kumtoa mwari katika makabila ya Wazaramo na Waruguru. Anabainisha kuwa, nyimbo hizo huchukua maudhui mazito mazito ambayo huonesha maisha yaliyomo katika jamii, migogoro na matatizo mbalimbali yanayozuka katika jamii. Kazi hii, ilimsaidia mtafiti kuelewa nyimbo zinazoimbwa katika harusi. Pia kazi hii, ilitafautiana na utafiti huu kwa vile,

iliangalia sherehe za harusi katika makabila ya Wazaramo na Waruguru. Kwa upande wake, utafiti huu umeegemea katika kuonesha namna kauli za nasaha zinavyojenga uhusiano wa wanandoa.

Coppens (1980), alitafiti ada za harusi za kisiwa cha Lamu, Kenya. Aliangalia baadhi ya nyimbo zinazoimbwa katika harusi za Waswahili wa Lamu na ameonesha namna nyimbo hizo zinavyowasilishwa katika harusi. Kazi ya Coppens ilimsaidia mtafiti kuzijua ada za harusi kupitia nyimbo za harusi za Lamu. Hata hivyo, kazi hii ilimtia ari mtafiti ya kutaka kujua kauli za nasaha zinajengaje uhusiano wa wanandoa.

Abdulla (2016), alitafiti athari za itikadi katika nyimbo za harusi za Kizanzibari. Katika utafiti huo alibainisha kuwa nyimbo za harusi huimbwa katika mazingira tafauti kama vile, kipindi cha kuwekwa harusi ndani, muda wa kurudi kuchukua biharusi. Pia alionesha kuwa nyimbo za harusi za Kizanzibari zimechukua itikadi nyingi mfano kutilia umuhimu katika kuheshimu ndoa, usafi, mashirikiano pamoja na kukaribisha wageni. Kazi ya Abdulla ilimsaidia mtafiti kuelewa itikadi zilizomo katika nyimbo za harusi wakati utafiti huu uliangalia kauli za nasaha zinavyojenga uhusiano wa wanandoa.

Muhammed (2007), aliangalia athari ya nyimbo za harusi kwa mke na mume. Alionesha namna nyimbo hizo zinavyowaathiri wanandoa hao huku zikiwaongoza juu ya kupendana na kuheshimiana. Miongoni mwa nyimbo hizo zimo nyimbo za singo ambazo huimbiwa mwari wakati wa kusingwa. Hata hivyo, Muhammed hakuangalia jinsi kauli za nasaha zinavyojenga uhusiano wa wanandoa kwa kutumia mifano ya harusi za Wapemba.

Suleiman (2015), alichunguza kiwango cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba katika miktadha tofauti kama vile katika kilimo, uvuvi, msiba pamoja na harusi. Alibaini kuwa msamiati wa harusini umebadilika kutokana na athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia yaliyopo. Sababu nyengine ni muingiliano wa watu wanaokuja kutoka katika sehemu mbalimbali zilizo nje ya mipaka ya jamii iliyotafitiwa. Kazi ya Suleiman ilichunguza mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba tafauti na utafiti huu ambao uliangalia kauli za nasaha katika harusi zinavyosimamia uhusiano katika ndoa.

2.2.2 Kauli za Nasaha katika Mila na Desturi za Harusi

Kavugha (1997), alichunguza mila na desturi za Wapare katika shughuli zao za harusi na alibaini kuwa katika kabila la Wapare siku ya harusi huwa ni siku ya shangwe. Ndugu, jamaa na marafiki wa harusi hufika nyumbani kwa bwanaharusi kwa shangwe huku wakiimba nyimbo. Utafiti wa Kavugha ni tafauti kabisa na utafiti huu kwa sababu aliangalia mila na desturi za Wapare katika harusi zao, ilhali, mtafiti wa kazi hii alijikita zaidi katika kuangalia kauli za nasaha katika harusi na matokeo yake katika uhusiano wa wanandoa.

Farsy (1967), alishughulikia ada za harusi katika kisiwa cha Unguja. Alifafanua kuwa, harusi hizo huanza na posa, kupeleka mahari, kusingwa kwa maharusi mpaka kufikia kufungwa kwa ndoa. Utafiti wa Farsy ulimsaidia mtafiti kujua miktadha ya nasaha katika harusi za Wapemba.

Gora (2015), alishughulikia utani katika sherehe za harusi za Watumbatu kwa kuangalia aina, sababu na taashira zake. Utafiti umebaini kuwa kuna aina nyingi za

utani katika jamii ya Watumbatu kama vile, utani wa mashemegi, marafiki, binamu na bibi au babu na wajukuu zake. Utani huu kwa desturi husaidia katika kuwasilisha mambo mazito ambayo katika mazingira ya kawaida yasingeweza kuwasilishwa. Ilivyo hasa, utafiti wa Gora ulisaidia kuelewa utani unaofanyika katika harusi za Watumbatu. Kwa upande wake mtafiti wa kazi hii aliangalia kauli za nasaha katika harusi za Wapemba zinavyojenga uhusiano wa wanandoa.

Ameir (2007), amechunguza maadili yanayopatikana katika nyimbo za ukungwi. Miongoni mwa nyimbo hizo ni kama zile zinazoimbwa kwa kuhimiza usafi, heshima, kumtunza mume, kuhusu starehe na stahamala. Naye Harries (1965) aliangalia utaratibu wa posa kwa jamii ya Waswahili na kusisitiza kuwa mshenga ni mtu muhimu katika utaratibu wa ndoa na hata kupanga sherehe ya harusi. Mshenga ndiye anayehusika moja kwa moja kupeleka barua huku akiwafanyia utani wale wakwe wa upande wa pili bila kuvuka mipaka. Kwa ujumla kazi ya Ameir ilimsaidia mtafiti kuelewa nyimbo za ukungwi namna zinavyotoa mafunzo kwa maharusi na katika kazi ya Harries ilimsaidia kujua namna ya posa zinavyoanza katika jamii ya Waswahili. Hata hivyo, maandiko haya, yamemtia hamasa mtafiti ya kuchunguza uhusiano wa wanandoa unavyojengwa na kauli za nasaha katika harusi za Wapemba.

2.3 Pengo la Utafiti

Licha ya kwamba mada zinahusu harusi zimeshatafitiwa sana hususani katika muktadha wa nyimbo. Baada ya mtafiti kuyapitia marejeleo ya watafiti waliyotangulia na kuona kuwa hawajajikita katika kuangalia uhusiano unaojengwa

na kauli za nasaha katika harusi za Wapemba. Hivyo, mtafiti aliliona pengo ambalo linahitaji kuzibwa na kuamua kuliziba pengo hilo kitaaluma.

2.4 Nadharia ya Uchambuzi Makini wa Matini (Critical Discourse Analysis)

Utafiti huu ulitumia nadharia ya uchambuzi makini wa matini. Nadhari hii ilianzishwa na Norman Fairclough (1995), ambayo huchunguza lugha katika mfumo wa matendo tofauti ambayo hufanywa katika jamii. Fairclough ameeleza kuwa lugha hutumika kuonesha uhusiano uliopo wa maisha ya jamii. Ameelezea kwamba nadharia hii hujumuisha misingi saba katika kuchambua matini, nayo ni:-

Msingi wa kwanza umeangalia lugha kama mfumo wa jamii na utamaduni wake katika kuchunguza uhusiano uliopo kati ya matini na jamii. Pili, mahusiano ya nguvu na mamlaka katika jamii hujengwa katika mfumo wa uhusiano uliopo katika utumizi wa lugha ndani ya matini. Tatu, matini huundwa na mambo makuu mawili ambayo ni jamii na utamaduni. Lugha ya jamii huathiriwa na utamaduni. Nne, matini hufanya kazi kubwa katika kujenga itikadi kwa kuonesha kuwa matini haiwezi kusimama peke yake lazima kuwe na itikadi zinazopambanua matini hiyo. Tano, uhusiano wa matini na historia ya jamii, matini haijitokezi katika ombwe bila kuwepo na mazingira na haiwezi kueleweka au kutafsirika vizuri isipohusishwa na mazingira ya jamii. Sita, wakati wa kuchambua matini ni lazima kuwepo na uwiano wa uhusiano baina ya matini na jamii inayochunguzwa. Nadharia ya uchambuzi makini wa matini ni jumla ya kufanya muunganiko kati ya mifumo ya kijamii. Msingi wa saba, unaeleza kuwa matini hutafsirika na kuelezeka. Nadharia ya uchambuzi makini wa

matini hukusudia kufafanua matini na ufafanuzi huo huweza kuwa wa namna mbalimbali kulingana na kiwango cha matini.

Nadharia hii huelekeza mambo muhimu ya kuzingatia katika kuangalia matini ambapo miongoni mwao ni muktadha na jamii. Pia wakati wa uchambuzi wa matini mwananadharia huyu alielekeza kuwa uchambuzi wa matini ni lazima ujikite katika maeneo makuu matatu ambayo ni kuangalia maandishi, kuchambua maandishi yenyewe na namna ya kuweza kuelezea jamii.

Nadharia hii pia ilielezewa na Widdowson (1995) aligusia mambo matatu wakati wa uchambuzi wa matini ambayo ni umuhimu wa muktadha, mada na uwakilishaji wa maudhui na mwisho asili ya urejelezi. Alitarajia kuwa uchunguzi wa vipengele hivi utashawishi kukubali kuwa wazo la matini ni kama muingiliano baina ya mwandishi na msomaji au mzungumzaji na msikilizaji katika kupata maudhui husika.

Pia Widdowson aliona kuwa uchambuzi wa matini una njia sita: Nadharia ya kitenda neni, maingiliano ya lughawiya ya jamii, mawasiliano yanayohusiana na mila na tamaduni za kabila, pragmatiki, uchambuzi wa mazungumzo na uchambuzi wa migawanyiko ya tofauti za kijamii. Kwa mujibu wa mwanadharia huyu vipengele hivi vinatofautiana lakini pia vinaingiliana na kulandana kwenye baadhi ya mambo muhimu. Miongoni mwa mambo hayo yameelezwa na Schiffrin (1984) ambayo ni uhusiano baina ya muundo pamoja na kazi vijenzi, matini na muktadha, misemo na mawasiliano.

Widdowson ameeleza kuwa mtazamo wa kuiangalia matini ni njia endelevu. Katika kulifanikisha hili mtafiti aliona kwamba msemeshwaji hutarajia kufahamu ujumbe wa mzungumzaji katika mazingira ya kawaida na katika njia inayotarajiwa. Mtafiti aligundua kuwa uchambuzi wa matini unahitaji umakini na mazingatio ya muktadha kwa mujibu wa matukio yanayojiri. Muktadha huhusiana na mijengeko ya maneno yanaweza kuwa ya lughawiya au la kwa kuihusisha na vipimo vya kawaida vya jamii hiyo. Naye Hymses (1964) alitoa wito kwa wanaoshiriki katika matendo mbalimbali ya mazungumzo kumfahamu mzungumzaji na anachokizungumza. Uewalewa wa kumfahamu mzungumzaji katika matukio ya kimawasiliano humuwezesha mchambuzi wa matini kufukiria ni aina gani ya mtu anaezungumza. Uwelewa wa mpokeaji wa matini humuwezesha mchambuzi wa matini kujua matarajio ya baadae.

Nadharia hii imetumika tangu mwanzo hadi mwisho wa utafiti huu. Katika misingi saba ya nadharia hii, imetumika misingi miwili tu. Lengo la utafiti la kwanza ambalo ni kuainisha kauli za nasaha anazopewa biharusi na bwanaharusi kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wapemba, mtafiti aliutumia msingi wa nne wa nadharia hii ambao unaeleza kuwa matini hufanya kazi kubwa katika kujenga itikadi kwa kuonesha kuwa matini haiwezi kusimama peke yake lazima kuwe na itikadi zinazopambanua matini hiyo.

Pia mtafiti ametumia msingi wa pili wa nadharia ambao ni mahusiano ya nguvu na mamlaka katika jamii hujengwa katika mfumo wa uhusiano uliopo katika utumizi wa lugha ndani ya matini. Msingi huu ulisaidia kutengeneza lengo la pili la utafiti

ambalo ni kufafanua uhusiano wa ndoa unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi.

2.5 Muhtasari wa Sura

Sura hii imeelezea mapitio ya maandiko ambayo yametumika katika utafiti uliofanyika. Maandiko hayo yametupa mwanga katika kuangalia kauli za nasaha kwa biharusi na bwanaharusi pamoja na uhusino unaojengwa na kauli hizo kwa maharusi katika jamii Wapemba. Pia kiunzi cha nadharia ya uchambuzi makini wa matini kimejadiliwa ndani ya sura hii, namna kilivyoongoza utafiti mwanzo mpaka mwisho. Sura inayofuata inaelezea mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti huu

SURA YA TATU

MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu mbinu zilizotumika katika utafiti uliofanyika.Vipengele vilivyohusi shwa hapa ni mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, sampuli na usampulishaji, mbinu za kukusanyia data, vifaa vya kukusanyia data, uchambuzi wa data, uthibiti na kuaminika kwa data pamoja na miiko ya utafiti.

3.2 Mkabala wa Utafiti

Kwa mujibu wa Enon (1998) ameeleza kuwa mkabala usio wa kiidadi ni mbinu ya kuchanganua data ambayo mtafiti hueleza na kufafanua data zake kwa njia ya maelezo. Katika utafiti huu mtafiti ametumia mkabala wa kimaelezo katika kufafanua data alizozipata kutoka kwa watoa taarifa ili kufikia lengo la utafiti.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti ulifanyika katika kisiwa cha Pemba, katika Mkoa wa Kusini Pemba: kwenye wilaya ya Chake Chake na wilaya ya Mkoani. Katika wilaya ya Chake Chake, utafiti ulifanyika katika jimbo la Chonga katika shehia za Chonga na Matale. Kwa upande wa wilaya ya Mkoani, utafiti ulifanyika katika jimbo la Chambani, shehia ya Dodo iliyopo Pujini. Mtafiti alichagua maeneo haya kwa sababu alishapata fununu kuwa kwenye maeneo haya mara nyingi wanandoa hupewa kauli za nasaha wakati wa harusi. Halikadhalika, mtafiti aliwahi kupata habari kwamba wakaazi wa maeneo haya wanayo desturi ya kutoa mashirikiano mazuri katika kazi za utafiti. Fununu

hizo zilikuwa sahihi na kwamba mtafiti alipokuwa nyanjani ilikuwa rahisi kwake kuipata data kutokana na mashirikiano ya watoa taarifa.

3.4 Sampuli na Usampulishaji

Kothari (2009) amefafanua kuwa sampuli ni sehemu ya jamii ya watu au vitu kwa ajili ya kutoa taarifa zitakazokuwa kiwakilishi cha jamii nzima.

Usampulishaji ni kitendo cha kuchagua sampuli ya kukusanyia data kwa kuchagua idadi ndogo ya wawakilishi kutoka katika kundi kubwa la watu au sehemu (Enon 1998)

3.4.1 Usampulishaji

Utafiti ulitumia usampulishaji lengwa ili kupata watoa taarifa walio na sifa alizozilenga mtafiti. Watoa taarifa hao ni mashekhe ambao hufungisha ndoa. Wanandoa wakongwe waliyomo katika ndoa kuanzia miaka kumi na kuendelea pamoja na wanandoa ambao wamefunga ndoa katika miaka ya karibuni. Pia makungwi na walimu wa kike wa madrasa ambao wanaotoa kauli za nasaha kwa maharusi.

3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa

Sampuli hii ilijumuisha jumla ya watafitiwa thelathini (30). Mashekhe watatu (3) wanaofungisha ndoa, kila shehia alichaguliwa shekhe mmoja. Wengine walikuwa makungwi watatu (3) ambao kila shehia alichaguliwa kungwi mmoja. Walimu watatu (3) wa kike wa madrasa wanaotoa kauli za nasaha kwa maharusi kila shehia

alichaguliwa mwalimu mmoja ambao walipatikana kwa njia ya kukusudia. Sampuli nyengine ilikuwa ni wanandoa ishirini na moja (21) ambao walikuwa wanandoa waliooa na kuolewa kwa muda mrefu kuanzia miaka kumi (10) na kuendelea, walihusishwa watafitiwa kumi na moja (11). Wanaume walikuwa watano (5) na wanawake sita (6). Watafitiwa walikuwa umri wao ni kuanzia miaka arubaini na tano (45) na kuendelea. Pia wanandoa waliooa na kuolewa karibuni walikuwa kumi (10), wanaume watano (5) na wanawake watano (5), ambao walichaguliwa watafitiwa wenye umri wa miaka ishirini (20) hadi thelathini na tano (35). Misingi ya kuchagua idadi ya sampuli ya watafitiwa katika utafiti imetokana na mawazo ya Enon (1998) na Kothari (2009), wanaeleza kuwa idadi ya sampuli katika utafiti wa kitaamuli haitakiwi kuwa kubwa mno au ndogo sana. Inatakiwa kuwa ya wastani kutokana na sababu tofauti kama vile, gharama na muda. Kwa hiyo, idadi ya sampuli hii ambayo ilikisiwa, ilitosheleza katika kusaidia kupatikana kwa data sahihi zilizohitajika.

3.5 Mbinu za Kukusanyia Data

Data ya utafiti huu ilikusanywa kupitia uwandani kwa kutumia mbinu tofauti. Mbinu zilizotumika ni dodoso, ushuhudiaji na usaili.

3.5.1 Dodoso

Mtafiti alitumia mbinu hii kwa kutengeneza maswali yaliyoendana na malengo ya utafiti. Jumla ya dodoso kumi (10) zilitolewa kwa watafitiwa ambapo walihusishwa wanandoa ambao wameoana miaka ya karibuni, wanaume watano (5) na wanawake watano (5). Katika mbinu hii mtafiti alishirikisha watafitiwa wanaoelewa kusoma na kuandika. Mtafiti aliwateua hawa kwa sababu walikuwa ni wepesi wa kuweza

kuandika taarifa sahihi zenye kufahamika. Pia watafitiwa waliweza kuandika taarifa kwa wingi zaidi kwa vile ilikuwa ni siri baina yao na mtafiti. Mtafiti alitumia mbinu hii kuwataka maharusi wataje kauli za nasaha walizopewa kipindi cha harusi. Hii ilisaidia kukamilisha lengo la kwanza la utafiti ambalo lilikuwa ni kubainisha kauli za nasaha kwa biharusi na bwanaharusi kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wapemba.

3.5.2 Usaili

Kupitia mbinu hii mtafiti alifanya mazungumzo ya ana kwa ana na watafitiwa akiwa uwandani baada ya kupata ridhaa zao. Mbinu hii ilihusisha watafitiwa ishirini (20), wanaume nane (8) na wanawake kumi na mbili (12) ambao wametoka katika kundi la Mashekhe watatu (3), makungwi watatu (3), walimu wa kike wa madrasa watatu (3) wanaotoa kauli za nasaha kwa maharusi na wanandoa waliyomo katika ndoa kwa muda mrefu (wakongwe) ambapo wanaume walikuwa watano (5) na wanawake sita (6). Usaili ulifanyika faragha ili kumpa fursa kila mmoja kujieleza bila woga. Kila kundi lilitakiwa kutoa kauli za nasaha wanazowapa maharusi au walizopewa kipindi cha harusi. Majibu yao yalisaidia kujibu suali la kwanza la utafiti lilohusu kubainisha kauli za nasaha anazopewa biharusi na bwanaharusi kwa mujibu wa utamaduni wa Wapemba.

Mtafiti aliwasaili mtu mmoja mmoja. Simu ya mkononi ilitumika kurikodi mazungumzo hayo, pia kalamu na daftari vilitumika kunakili baadhi ya taarifa. Mbinu hii ilimsaidia mtafiti kupata taarifa za ziada ambazo asingaliweza kuzipata kupitia njia nyengine. Hii ni kwa sababu katika usaili watafitiwa hutokea

kuzungumza maswala mengi kwa kina zaidi ya matarajio ya mtafiti. Pia watafitiwa walionesha mashirikiano mema ya utowaji wa taarifa wakati usaili ulipofanyika na walipewa uhuru wa kueleza kile ambacho mtafiti aliwahoji.

3.5.3 Ushuhudiaji

Kupitia mbinu hii mtafiti alihudhuria hafla kumi na mbili katika maeneo teule ya utafiti, Katika maeneo hayo mtafiti alihudhuria katika shughuli za uradi, singo, ndoa na siku ya vyombo. Data iliyopatikana ilisaidia kujibu lengo la kwanza la utafiti. Simu ya mkononi ilitumika kurikodi taarifa zilizohitajika wakati wa ushuhudiaji. Mtafiti alitumia mbinu hii ili kuona uhalisia wa kauli za nasaha zinazotolewa na wanafamilia.

3.6 Vifaa vya Kukusanyia Data

Utafiti ni mchakato ambao unahitaji matayarisho ya vitu mbalimbali ili kufikia katika mwisho ulio nzuri. Vifaa vyengine ambavyo vilitumika katika utafiti huu ni kompyuta na flashi.

3.7 Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Data za utafiti huu zilichanganuliwa kwa njia ya maelezo. Kupitia mkabala huu, mtafiti alichanganua kauli za nasaha za harusi ili kutimiza malengo ya utafiti huu. Data zilizokusanywa zilichanganuliwa kwa kufuata hatua zifuatazo:

a. Mtafiti alisikiliza data iliyokuwa imerikodiwa kwenye simu. Pia alitalii maelezo ya watafiti aliyoyaandika kwenye daftari lake maalum kwa kazi hii.
b. Data ya kwenye simu na ya kwenye daftari ilinukuliwa kwenye kompyuta.

c. Hatua iliyofuata ilikuwa ni kuainisha data kwa kutumia kigezo cha kauli za nasaha alizopewa biharusi na zile za bwanaharusi. Hatua hii ilitimiza matlaba ya lengo la kwanza la kuainisha kauli za nasaha.

d. Kwa kutumia maelezo ya watafitiwa, mtafiti alichanganua jinsi kauli za nasaha zinavyojenga uhusiano baina ya mke na mume katika jamii ya Wapemba. Hatua hii ilitimiza lengo la pili ambalo lilikuwa ni kuchunguza uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi katika jamii ya Wapemba.

3.8 Uthibiti na Kuaminika kwa Data

Taarifa za utafiti huu ambazo zilikusanywa zilikuwa za kweli na zenye kupimika katika utafiti uliokusudiwa. Data zimekusanywa na kuchanganuliwa kutokana na malengo mahsusi ya utafiti huu. Pia mtafiti aliweka bayana uchambuzi wa data kwa kutumia maelezo yenye kueleweka.

3.9 Miiko ya Utafiti

Jambo moja muhimu ambalo mtafiti wa kazi hii alilizingatia ni kufuata maadili ya utafiti vile ipasavyo. Hivyo basi, mtafiti kabla ya kufanya maamuzi ya kwenda uwandani, kwanza alilazimika kuomba idhini katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Halikadhalika, katika kuchunga maadili ya utafiti, mtafiti alijitahidi kuwa muwazi, muadilifu, muaminifu na kwamba alihakikisha kuwa alichunga siri za watoa taarifa wake kama walivyokubaliana. Zaidi ya hayo mtafiti aliomba ridhaa kwa kila mtoa taarifa pale ambapo alihitaji kunasa sauti zao. Inafaa ieleweke kuwa wakati mtafiti anakutana na watoa taarifa hawa alijaribu vyema kutumia lugha ya upole

hususani pale alipojitambulisha, na hivyo alijieleza kwa ufasaha yeye ni nani, anatoka chuo gani na kwa nini yupo mahala hapo.

3.10 Muhtasari wa Sura

Sura hii imetusaidia kupatikana eneo la utafiti pamoja na watafiti. Watafitiwa walitoa data ambazo zilikamilisha utafiti huu. Data zilizokusanywa maswali yake yalihusishwa na malengo mahsusi na zilikuwa sahihi zenye kuaminika. Pia mtafiti alichunga maadili ya jamii. Sura ya nne inahusu uwasilishaji na uchambuzi wa data.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA

4.1 Utangulizi

Sura hii inahusu uwasilishaji wa data na kujadili matokeo ya utafiti uliofanyika kuhusu Kauli za Nasaha katika Harusi Zinavyojenga Uhusiano wa Wanandoa. Sura hii imeanza na utangulizi. Baadae ikaorodhesha kauli za nasaha za biharusi na bwanaharusi pamoja na kuzifafanua. Halafu ikaonesha uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi. Mwisho sura hii ilimalizia na muhtasari wa yaliyojadiliwa.

4.2. Uainishaji wa Kauli za Nasaha

Kauli za nasaha zilizoainishwa hapa zilikusanywa kupitia posa, uradi, singo, ndoa na siku ya vyombo. Kulikuwa na kauli zilizomuhusu biharusi na zilikuwepo zilizomuhusu bwanaharusi. Uainishaji ulikuwa hivi ifuatavyo:

4.2.1 Kauli za Nasaha za Biharusi

Kwa Wapemba, mara tu baada ya kukamilika kwa posa, maandalizi ya harusi huanza. Kwa mtoto wa kike huwa hana ruhusa ya kutoka kwenda sehemu yoyote isipokuwa kwa dharura maalumu. Hapo hufuatanishwa na mtu wake wa karibu tena mwenye kuaminiwa katika familia ili ampeleke sehemu husika pamoja na kumrudisha nyumbani katika hali ya usalama. Kwa wakati wa sasa hali hiyo inaonekana kupungua kasi. Watoto wa kike aghlabu huwa na harakati tafauti za kimaisha zikiwemo za kwenda kazini na hata vyuoni. Hivyo, kuwekwa ndani au

kufuatanishwa na watu katika safari zao huwa ni jambo lisilowezekana. Hata hivyo, wasaa unapopatikina hupewa kauli za nasaha kwa ajili ya kuwaandaa kwa ndoa.

4.2.1.1Kauli za Nasaha katika Posa

Katika kipindi hiki, wazazi hasa wa kike pamoja na jamaa wa karibu wa familia kama vile mabibi, shangazi, mama wadogo, dada huwa karibu na biharusi mtarajiwa na kumpa kauli za nasaha zinazohusu mambo ya ndoa. Baadhi ya kauli za nasaha anazopewa biharusi ambazo mtafiti alizipata ni hizi zifuatazo:

"Jitahidi sana na haya tunayokunasihi, mwanamke ni usafi, nakunasihi ujitahidi na usafi, usafi ndio kila kitu."

Kauli ya nasaha hii ilipatika kupitia ushuhudiaji katika kijiji cha Chanjamjawiri Melinne wakati mwalimu wa kike wa madrasa pamoja na familia ya biharusi mtarajiwa wakimpa kauli za nasaha biharusi juu kudumisha usafi. Mwalimu alimnasihi biharusi kwa kumwambia mojawapo ya tabia njema kwa mke kuwa nayo ni unadhifu. Mke anatakiwa adumishe usafi katika mazingira yote ya nyumba yake. Pia mume wake amuweke katika hali ya usafi kwani usafi huficha kila kitu kama vile umaskini. Mume anapoonekana yuko katika hali ya uchafu basi, mara nyingi jamii ya Wapemba humtia dosari mke na kusemwa kuwa hamshughulikii mume wake. Usemwaji huo huja kwa sababu katika jamii hii mke ndiye anaetambulika kuwa ni mwenye dhamana ya kumuandaa mume kwa kumnadhifisha vizuri kimwili na kimavazi. Ndiyo maana pale itokeapo mume kuwa mnadhifu basi, husemwa kwamba 'fulani ameoa'. Pia usafi kwa mwanamke ndilo jambo linalomjengea hadhi siyo tu kwa mumewe na kwa jamii iliyomzunguka'. Mwalimu aliendelea kusema kwamba

‘hata, dini yetu ya Kiislamu nayo inatuhimiza suala la usafi wa mwili, kauli, mavazi pamoja na matendo’.

“Sikiliza vyema haya tunayokunasihi, ndoa ni sawa na chungu kilichopo katika mafya matatu.”

Hapa kwanza tunaileta maana ya jifya kama ilivyoandikwa kwenye BAKIZA (2010) mojawapo ya mawe matatu yanayoinjikiwa chungu. Likiwa moja huitwa jifya na wingi wake ni mafya. Mtafiti alipomsaili mwalimu wa kike wa madrasa katika kijiji cha Kichanjaani Pujini juu ya makusudio ya kauli ya nasaha hii alieleza kuwa, makusudio ya kusemwa kuwa ndoa ni sawa mafya matatu imekusudiwa wanandoa, wazazi na jamii. Yaani, jifya la kwanza linachukua nafasi ya mke na mume. Jifya la pili ni wazazi wa mke na mume na jifya la tatu ni jamii iliyowazunguka na chungu ni ndoa. Kauli ya nasaha hii hupewa biharusi mtarajiwa ajue kuwa ili ndoa yake ikae sawa na salama ni muhimu mihimili hii iwe madhubuti, yaani wanandoa (mke na mume), wazazi wote wa pande mbili pamoja na jamii. Kwa hiyo, ndoa ili iwe sawa na salama inategemea mafya matatu na kama jifya moja likiondoka mara nyingi husababisha ndoa au chungu hicho kuingia kwenye misukosuko. Mwalimu aliendelea kueleza hapa tunaona kuwa ili uimara wa ndoa upatikane ni lazima mume na mke, wazazi wa mke na mume na jamii yote iwe kitu kimoja katika kuiengaenga ndoa ya watoto wao ili pasije pakatokea fitina ikapelekea kuharibika kwa ndoa hiyo. Kwa hiyo, mtafiti aligundua kuwa kauli za nasaha Upembani zina mchango mkubwa katika kuidumisha ndoa.

“Sikiliza vizuri tunayokwambia, unapotoka kwenda safari uombe ruhusa mke hatakiwi kutoka bila ya ruhusa ya mumewe.”

Katika usaili na mtafitiwa katika kijiji cha Tondooni Pujini alieleza kauli ya nasaha hii hutolewa kwa biharusi mtarajiwa ili imkanye tangu mwanzo aache tabia ya kutoka na kwenda sehemu yoyote bila ya kupata idhini kutoka kwa mume wake. Ruhusa hiyo aombe kabla ya siku ya safari, siyo aombe baada ya kuvaa nguo kwa ajili ya kutoka kwenda safari. Hali hii haichukuliwi kuwa ameomba ya ruhusa bali husemwa kuwa ametoa taarifa. Kwa hiyo, mke mtarajiwa huambiwa hivyo ili aombe ruhusa mapema kabla ya siku ya safari kuwadia.

Mtafitiwa aliendelea kueleza jambo hilo ni muhimu kwa sababu pale mke anapoomba ruhusa mapema, mume anaondokana na wasi wasi na anajua mke wake yuko sehemu fulani na salama. Pia huwa ni njia mojawapo ya mke kwa mumewe kumuonesha utiifu na kumjali. Hivyo, mume huzidisha mahaba na kumtunza mkewe. Wala huwa hayupo tayari kushawishiwa au kujazwa fitina na watu wengine. Kwa sababu huwa anaelewa mwenendo na utaratibu nzima wa mkewe. Kusema kweli, jambo hili la kuomba ruhusa mapema hekima yake ni kuwapatia uhuru wale waume wenye wivu katika kujiandaa kwa kufanya uchunguzi wa safari za wake zao.

“Tahadhari sana, wivu kupita kiasi ni tatizo katika ndoa yako.”

Mtafiti alimsaili mtafitiwa wa kijiji cha Dodo Pujini alieleza kwamba, moja miongoni mwa kauli ya nasaha adhimu na muhimu kwangu na siwezi kuisahau katu ambayo nilipewa na mmoja miongoni mwa watu wa familia yangu ni ‘kupunguza wivu wa kupitiliza’. Alielezwa kuwa katika maisha ya ndoa wivu hauwezi kuepukika. Wivu ni suna kufanyiana mke na mume ila usichupe mipaka. Wivu ukizidi mno huleta madhara makubwa katika maisha ya ndoa. Wakati mwengine hupelekea kuzuka kwa mgogoro baina ya mke na mume katika ndoa yao, chanzo ni

wivu ulio pindukia mipaka. Hivyo, mke na mume hunasihiwa kulainisha wivu wao ili ndoa iwe salama bila ya kuitia dosari. Mtafiti aligundua kuwa wivu unaochupa mpaka mara nyingi mtu huweza kujenga hisia za vitu ambavyo havipo na kuhatarisha usalama wa ndoa. Kiasi ambacho inayumkinika kwa wanandoa hao kuweza kuachana au kujeruhiana.

“Nakunasihi tena shikilia vyema nikwambiayo, ukiwa katika ndoa usikilize maneno ya watu, waache watu na mambo yao na ushughulikie yako.”

Kauli hii ya nasaha ilipatikana kutoka Kijiji cha Dodo Pujini wakati mtafiti akimsaili mtafitiwa alieleza kuwa maisha ya ndoa huandamana na mambo mengi. Kuna baadhi ya watu katika jamii hujipanga kwa ajili ya kutia fitina tafauti kwa mke au mume na kusababisha ugomvi, hatimaye huweza kupelekea kuachana. Ni vizuri mke na mume kuwafahamu wanajamii wale ambao ni wema ili washikamane nao na wabaya ili kujiepusha nao. Pia wanandoa wanapopewa maneno ya fitina na watu wasikurupuke na kuanza kuvamiana kwa kugombana au kupigana. Muhimu kupitisha uchunguzi wa kina juu ya jambo hilo. Hata ikigundulika kuwa jambo hilo lina ukweli, basi wasiwe na jazba wafanye suluhu kwa kutumia hekima na busara ili waendeleze maisha yao ya ndoa. Kwani wakifanyiana ghadhabu, kila mmoja kwa mwenzake kunaweza kupelekea kulegalega au kukatika kwa ndoa. Baadhi ya waliohojiwa wengine pia walikiri kwamba zipo ndoa kadhaa ambazo zimevunjika kutokana na kushindikana kwa upatikanaji suluhu ulio nzuri. Kwa bahati, uchunguzi ulifanyika na ndipo ikajulikana kuwa ndoa katika jamii ya Wapemba huvunjika mara nyengine kwa sababu kama hizo.

“Jitahidi sana, uwe mwaminifu katika ndoa yako.”

Taarifa hii ilikusanywa kutoka kwa mwalimu wa kike katika kijiji cha Matale wakati aliposailiwa juu kauli za nasaha wanazowapa maharusi. Mwalimu alieleza kuwa humpa nasaha mke juu ya kujijengea tabia ya uaminifu katika ndoa yake. Uaminifu katika kuchunga na kushughulikia mali za mume. Isiwe mume ameweka kitu au pesa ndani, mke akaichukua pasi na kuomba ruhusa kwa mume. Kwa sababu siyo kila kitu ambacho mume hukileta ndani huwa cha kwake, inawezekana wakati mwengine kitu hicho ni amana tu alipewa. Hivyo, mke akiichukua amana hiyo inaweza ikapelekea matatizo kwake na kwa mumewe. Hili limebainika kuwa baadhi ya waume wengi pale wanapoanza tu kuowa huwa na tabia ya kuwapima wake zao kwa mambo mbalimbali. Miongoni mwa hayo mambo ni kuangalia uaminifu kwa wake zao. Kwa hiyo, mke akiwa muaminifu humfanya mume wake azidi kumuamini pamoja na kuondoa wasiwasi kwake.

“Zingatia vizuri haya tunayokwambia, mpe mume ahsante kwa kila zuri analokufanyia”.

Data hii ilipatikana kwa mwalimu wa kike wa madrasa kutoka Matale aliposailiwa na mtafiti. Mwalimu huyu wa kike alieleza huwapa kauli za nasaha maharusi juu ya kulitumia neno ‘ahsante’. Ahsante ni neno dogo kwa kulitamka. Lakini lina hadhi na haiba kubwa kwa aambiwae. Kutokana na kutambulikana thamani ya neno hili, ndipo mke mtarajiwa humnasihi kulikariri kila mara pale anapoletewa zawadi au kuambiwa maneno mazuri kutoka kwa mumewe. Neno ‘ahsante’ linapotumika ipasavyo, huchangia katika udumishaji wa ndoa. Kwa hiyo, mke humnasihi sana kuitumia ‘ahsante’ kwa lolote zuri analofanyiwa na mume wake hata kama dogo. Mwalimu aliendelea kueleza ‘ahsante’ humletea mume furaha, kuona anaheshimiwa,

anajaliwa na kuthaminiwa na mke wake. Pia mume anapata moyo na nguvu ya kukutekelezea jengine zaidi ya lile alilokufanyia. Hata hivyo, mume naye anapofanyiwa jambo zuri na mke wake ni vyema atowe ‘ahsante’ ili moyo wa mke nao ukunjuke, ufarajike na uvutike naye.

“Tunakunasihi biharusi mtarajiwa, uwe mcheshi, mchangamfu na mstaarabu kwa mumeo, jamaa zake na majirani wala usioneshe jeuri na majivuno kwao.”

Mtafiti alimsaili mwalimu wa kike wa madrasa kutoka kijiji Kipapo Chonga alizungumza kuwa humpa kauli za nasaha biharusi mtarajiwa kumuonya ajiepusha na tabia mbaya ya ujeuri, ujuba na kujiona mambo haya si mazuri mke kuwa nayo. Wapo baadhi ya wanandoa, kabla ya kufungishwa ndoa, huwa ni wazuri na wema. Hivyo basi, biharusi mtarajiwa humnasihi awe ni kigezo chema katika kuienzi ndoa yake kwa kujitahidi asiwe fedhuli kwa mumewe, jamaa wa mumewe, majirani na wengineo. Kwa sababu watu husema kuwa ‘dharau haijengi, hubomoa’. Humnasihi kuishi na watu vizuri kwa sababu wao ndio walinzi wa ndoa yake pindi akikaa nao kwa wema. Pia wanaweza kumjengea mazingira mabaya katika ndoa ikiwa hakuishi nao vizuri.

“Jihadhari sana, ufanye kile akitakacho mume na anachokukataza uachane nacho.”

Kauli ya nasaha hii ilipatikana mtafiti alipomsaili mtafitiwa wa Tondooni Pujini alieleza kuwa, aliambiwa kwamba, mke bora ni yule mwenye tabia ya kutii amri za mume wake zilizo za kheri anapoamrishwa kwa kuzitekeleza bila ya pingamizi ili kujenga ndoa bora. Pia mke hutakiwa ajiepushe na kutenda kile ambacho mume amemkataza kwa kuepusha matatizo. Mfano, aliambiwa kama aliomba ruhusa kwa mume wake ya kwenda sehemu fulani na akaruhusiwa. Mke akajiandaa muda

ulipowadia wa kwenda safari yenyewe, mume akaghairi na kumwambia mke wake asitoke tena kwenda safari. Basi mke alielezwa kuwa haimpasi kulazimisha kuwa lazima atoke kwenda safari hiyo. Kwa sababu jambo hilo linaweza kupelekea kutokea madhara ambayo hayakutarajiwa. Kwa hiyo, mke mtarajiwa hunasihiwa abakie nyumbani tena pasi kukasirika ikawa ugomvi, achukulie kitu cha kawaida, amekosa leo ruhusa, anaweza mume akakuruhusu siku nyengine.

“Sikiliza vyema haya tunayokunasihi, uwe mkweli na muwazi kwa mumeo.”

Mtafiti alipokuwa uwandani alimsaili mwalimu wa kike Kichanjaani alizungumza kauli ya nasaha hii humpa biharusi mtarajiwa kama ni njia mojawapo ya kumtahadharisha, kuwa ndoa ni jambo jema sana. Kichochezi kimojawapo cha kuidumisha ndoa yako ni kuwa mkweli na muwazi kwa kila jambo. Unapo yadumisha mambo haya, uaminifu mkubwa unajengeka baina yako na mume. Ukweli na uwazi huo uanze pale panapotokea tatizo kati yenu, muambizane wala musifichane. Kwa mfano, kama kuna kitu miongoni mwenu mmoja alikifanya, ambacho labda sio kizuri, amueleze ukweli mwenzake. Jambo hili linaweza kuepusha shari ya tatizo liliyopo. Mke kuwa muwazi na mkweli ni njia nyengine ya kukatisha fitina za watu wasiyo wema. Pia ufichaji wa jambo hupelekea madhara huenda siku mmoja, anaweza kuja kugundua mmoja miongoni mwenu kwamba mwenzake ana jambo lisiloridhisha akaona kuwa anafichwa. Hatimaye, kurupushani za hisia mbaya zikaanza ikawa sababu ya kutokea kwa mgogoro juu ya wawili hao.

Kutokana na utafiti huu imedhihirika kwamba wakati wa posa biharusi hufundishwa usafi, kumtunza mume, kuaminiana, kushirikiana, kumtii mume, wivu wa kiasi,

ukarimu kwa mume na nduguze, kushukuru, kuridhika na kuimarishwa zaidi katika mambo ya upishi.

4.2.1.2 Kauli za Nasaha katika Ndoa

Mtafiti alikusanya kauli za nasaha zilizohusu maisha ya ndoa. Kauli hizo zilitolewa siku ya kufungwa ndoa kwa maharusi wapya. Kauli hizo ni hizi

"Jitahidi sana, mapambo yako yawe kwa ajili ya mumeo tu wala usijipambe ili kujionesha kwa watu wengine."

Mtafiti alimshuhudia biharusi katika kijiji cha Limani akipewa kauli ya nasaha na miongoni mwa watu familia aliambiwa kuwa asije akafuata tabia za wanandoa wengine katika jambo la kujipamba. Baadhi ya wanandoa wanapokuwa katika nyumba zao huwa hawajipambi lakini wanapotoka kwenda safari, ndio wanapojipamba. Biharusi alielezwa kuwa hiyo siyo tabia njema kwa mke kuwa nayo. Mke humpasa ajipambe kwa ajili ya mume wake na wala asioneshe mapambo yake kwa watu wengine. Kwa sababu pale mke anapojipamba nje ya nyumbani kwake, kuna madhara kadhaa yanaweza kutokea kama vile kufikwa na 'husda' zitokanazo na watu waovu au kupata laana ambazo hutoka kwenye ndimi za watu watukufu.

Baadhi ya watu hutokea kumsifia na mke huyo akashawishika kwa sifa hizo. Hatimaye, mke huvutika na hisia kali za watu hao na kufanya maamuzi ya kumuendea kinyume mumewe. Kwa hiyo, mke alinasihiwa anapotoka nje ya nyumba yake avae kawaida asitoke na mapambo. Inasemekana kwamba, mapambo yanaleta

ushawishi mkubwa kwa watu hasa wanaume wanaweza wakakufuata kwa nia iliyokuwa sio nzuri ikawa sababu ya kukuharibia ndoa yako.

“Nasaha zetu ni kwamba, mtu anapokuwa katika ndoa anatakiwa kujielewa.”

Mtafiti akiwa katika kijiji cha Chanjamjawiri, Njia ya Kidongo akimsaili mtafitiwa alieleza miongoni mwa kauli za nasaha alizopewa wakati wa kuingia katika ndoa. Aliambiwa kuwa mtu akiwa katika ndoa anatakiwa ajichunge na mambo mbalimbali mabaya ambayo yanapelekea kutia dosari ndoa yake. Kuachana na mambo ya utoto afahamu kuwa amekuwa katika daraja jengine la utuuzima. Pia ajuwe yupi mkubwa, mdogo na kuwawekea heshima. Vilevile, mke aheshimu wakwe, mawifi, mashemegi pamoja na majirani. Halikadhalika mke ajuwe yupi wa kumtania na yupi wa kumstahi. Kwa mfano, isitokezee kumtania mkwe wake yoyote kwa sababu tu watu wa mtaani humtania kwa kumwita jina la utani naye akaamua kumwita. Mke hatakiwi kuwatania wakwe zake.

“Mume anapokuja nyumbani hata kama una kazi au umekaa na wenzako barazani basi nakunasihi, acha shughuli zako umshughulikie mumeo kwanza.”

Mtafiti alipohudhuria katika maandalizi ya kumuandaa biharusi, kuingia katika maisha mapya ya ndoa katika kijiji cha Kidongo Matale, alimsaili dada wa biharusi juu makusudio kauli ya nasaha aliyoitoa kwa biharusi. Dada wa biharusi alifafanua kuwa hii ni kauli ya nasaha mojawapo muhimu sana. Mke mtarajiwa hupatiwa kauli ya nasaha hii ili kumtahadharisha na tabia za wanandoa wengine wenye tabia hiyo. Hunasihiwa kwa kuambiwa kuwa baadhi ya wanandoa huonesha dharau kwa waume zao. Kwa mfano, mke anaweza kumuona mume wake ameshafika nyumbani kutoka

katika harakati zake za kimaisha. Basi kwa dharau zake, huweza kuendelea kufanya shughuli zake au akaendelea kuzungumza na wenzake bila kujali.

Dada alimtahadharisha biharusi kuwa jambo hili siyo jema kulifanya ajiepushe nalo. Pia biharusi alinasihiwa kwa kuambiwa kuwa angalau kwanza ende kumuuliza hali pamoja na kumsikiliza kule atokako ni salama. Alisisitizwa kunasihiwa kuwa ni jeuri kubwa kwa mwanandoa kuhiyari mazungumzo ya barazani na kumuacha mume wake ndani akijihudumia mwenyewe. Hata hivyo, biharusi mtarajiwa huyo alizidi kuambiwa kuwa nasaha hii tuliyokupatia uizingatie ipasavyo. Siyo iwe tayari muna watoto wakubwa au mfanyakazi wa ndani, akamtumia yeye au wao (watoto) kwa kumuhudumikia mume wake. Jukumu hilo siyo lao. Kwa hivyo, mume ili ajenge upendo kwa mke, mambo kama haya mke ajiepushe nayo.

“Sikiliza kwa makini haya tunayokueleza, tena ukayafanyie kazi vizuri, ukawe mke mwema kwa mumeo, ukajitahidi kutunza heshima yake, uwatunze wazazi wake, jamaa zake pamoja na kila kitu chake.”

Kauli ya nasaha ilipatikana katika kijiji cha Sebunyemi Matale familia ya biharusi na baadhi jamaa wengine wakimpa kauli ya nasaha biharusi. Walimuelekeza mke mtarajiwa kutambua kuwa anadhamana ya kuangalia na kutunza mambo yote ya mume. Mume ndiye kiongozi wa juu katika familia na mshughulikiaji wa majukumu ya nyumbani, lakini msaidizi wake huwa ni mke ambaye humsaidia majukumu tafauti ya nyumbani. Hivyo, mke mtarajiwa aliambiwa ajitahidi kutekeleza dhamana zake ipasavyo ili kumpunguzia mume mzigo nzito wa majukumu. Pia mke ajipambe kwa sifa njema zinazompelekea kumjengea heshima mume wake katika jamii pamoja na familia yake waone kweli mtoto wao amepata mke mwema.

"Jitahidi sana, kumuomba msamaha mumeo pale unapomkosea, tena urudi matawi ya chini ili upate msamaha wake."

Kauli ya nasaha hii alielekezwa biharusi katika kijiji cha Uzunguni Chanjamjawiri alinasihiwa na watu wa familia yake kuwa ajitahidi kumuomba mume wake msamaha pale anapofanya kosa. Mke aombe msamaha huo akiwa katika hali ya unyonge ili kuonesha anataka asamehewe na mume wake. Wala mke asijitie kiburi akaona hana haja yoyote ya kutaka msamaha wa mume. Kwa sababu hasira za mume kwa mke huondosha ukaribu wa wanandoa hawa. Pia huenda ikawa sababu ya maisha ya mke kutonyooka ipasavyo. Hivyo mke ajitahidi kutumia njia nzuri kuhakikisha mume amekuwa radhi naye.

Pia baadhi ya waliohojiwa wenye mtazamo wa kidini katika kijiji cha Gereji, wameeleza kuwa mke pale akosapo radhi ya mume huwa ni changamoto nzito inayomkosesha pepo mke ambayo kila mja hutaka aipate pepo hiyo. Mnasaba kama huo ndiyo unaowafanya wazee, kumnasihi mwana wao kuwa mwepesi wa kuomba msamaha kwa kosa lolote litokealo kwenye maisha ya ndoa yao. Ingawa wakati mwengine, imebainika kuwa baadhi ya waume huwa wagumu hawapo tayari kusamehe wanapoombwa msamaha na wake zao, wanasahau kuwa mke naye ni binadamu asiye mkamilifu. Hivyo pale anapofanya kosa na kuomba radhi, ni vyema mume kusamehe mke wake.

"Tunakunasihi, mumeo anaponuna (anapokasirika) mke naye asinune."

Mtafiti alipohudhuria sherehe ya harusi, katika kijiji cha Pogwa Pujini alimshuhudia bibi mzaa mama wa biharusi akimpa kauli ya nasaha mjukuu wake, alimwambia

kuwa mke anapomuona mume hayuko katika hali ya kawaida naye asibadilike. Bali mke hutakiwa amuulize mumewe tatizo lililopo. Mke anapolijua tatizo basi atumie busara ili amtulize mume wake mpaka arudi katika hali yake ya kawaida. Pia mke mtarajiwa alinasihiwa kuwa atambuwe nafasi yake kwa mume; hasa nafasi ya uliwazaji. Mke aliambiwa kuwa maliwazo hufukuza hasira katika kila hali. Bibi alizidi kumsisitiza mjukuu huyo kuwa ikiwa wote wanakasirika, mambo hayawezi kwenda na tatizo bado linaendelea kuwepo. Zaidi alielezwa kuwa 'hasira hasara' na 'mmoja akiwa moto mwengine awe baridi'. Pia mke aliambiwa kuwa hakuna nyumba isiyo mivutano ila iwe ya kawaida na yenye kumalizika na waache tabia ya kununiana ili kujenga maisha mazuri ya ndoa.

"Tahadhari sana na ulimi, tunakunasihi, ulimi wako unatakiwa utumie vizuri. Maneno mazuri humtoa nyoka pangoni."

Mtafiti akiwa uwandani alimsaili mwalimu wa kike wa madrasa katika kijiji cha Kipapo Chonga juu ya kauli za nasaha anazowapa maharusi. Mwalimu alizungumza kuwa kauli ya nasaha hii ni muhimu ambayo hupewa mke mtarajiwa, aliambiwa kwamba ulimi ni kiungo kizuri pale mtu anapojua kukitumia. Pia kinakuwa kiungo kibaya pale anapokosa kukichunga. Katika dunia mtu anakuwa anastarehe na watu humpenda na kuwa pamoja naye, muda wote anakuwa mtu wa watu kutokana tabia njema ya kutumia vizuri ulimi. Aliendelea kumsisitiza mke namna ya kutumia vizuri ulimi kwa mume wake kwa kumpa maneno mazuri, ajuwe zuri la kumjibu mume wala asimjibu jeuri. Pia mke atumie ulimi vizuri kwa familia ya mume, majirani na jamii yote iliyomzunguka kwa wakubwa na wadogo. Mke mtarajiwa huyu alizidi

kumnasihi kwamba ikiwa anajua namna ya kutumia ulimi vizuri, basi ndoa inazidi kufana.

Kwa kawaida katika harusi za Wapemba baada ya harusi kukamilika wazazi wa familia mbili hukutana pamoja takribani huwa siku ya pili au ya tatu tokea ndoa kufungwa. Wazazi hawa hukutana kwa ajili ya kutambulishana, kujuana na kukabidhiana ulezi kwa vile huwa tayari wameshaunganisha udugu baina yao. Baada ya hapo pande zote mbili za familia hizo hutoa kauli za nasaha kwa bwanaharusi na biharusi zinazohusu namna ya kuishi kwa kuvumiliana na kustahamiliana katika maisha ya ndoa. Kutokana kuwa Waswahili husema ‘hakuna nyumba isiyo songwa ugali’ hii ina maana kwamba katika maisha ya ndoa hakuna mema matupu. Pia matatizo yanaweza kujitokeza, cha msingi wanandoa wenyewe wawe na subira na kuandaa mbinu bora ya kukabiliana nayo na kutengeneza mazingira mazuri ya kufanya utatuzi pindipo yakitokea. Vilevile siku hiyo huambatana na upelekaji wa mbanjo (sanduku) yaani ni zawadi anazopelekewa biharusi kutoka upande wa bwanaharusi kama vile nguo, viatu, mapambo na mengineo kama ni pongezi kwa biharusi na kumkaribisha katika ukoo mpya. Baadhi ya kauli za nasaha ambazo zilizopatikana katika siku ya vyombo ni:

“Zingatia kwa makini haya tunayokunasihi, usije ukaifanya familia ya mume ikagombana kwa ajili yako.”

Kauli ya nasaha hii ilishuhudiwa na mtafiti siku ya vyombo katika kijiji cha Mtondooni shehia Chonga baba mdogo wa biharusi alimfahamisha mtoto wake akae na wazazi wa mume vizuri na familia yake yote kwa kuwawekea heshima na kuwaona kama wazazi wake waliomzaa. Pia asigombanishe majirani, aheshimu

wakubwa na wadogo wote ili na wao wamjengee heshima. Baba mdogo aliendea kumnasihi mtoto wake kuwa asije akafanya vibaya ikawa watu wa mtaa wanamuoneshea vidole na kumuombea dua ya balaa ili aondoke mtaani pao kutokana na kuwafanyia wasioyapenda. Alimwambia ameolewa katika familia ambayo imefungamana na inapendana. Asije akaifarakanisha familia ikawa mbalimbali kila mtu na lake, mfungamano wao ukapotea kabisa. Vilevile, alimueleza mwanangu familia ikiwa imeachana jitahidi uiunganisha na kuwa kitu kimoja.

“Jihadhari sana, usimdai mumeo kitu ambacho hana uwezo nacho, uridhike na anachokupa.”

Mtafiti aliipata kauli ya nasaha kupitia siku ya vyombo au ya kukabidhiana ulezi katika kijiji cha Mjana Pweza Pujini, baba mdogo alimuonya mwanawe kutokuwa na tabia ya kutaka mambo makubwa apatiwe na mume wake. Baba mdogo alimtaka mwanawe apokee chochote kile anachopewa na mume wake kikiwa kizuri au kibaya, kikubwa au kidogo, kisha aridhike nacho aone huo ndio uwezo wa mume wake. Aliendelea kumwambia mke anapokuwa na tabia ya kuridhika huwa mtu mzuri, huwa hababaishwi na chochote anachokiona kwa watu wengine kutokana na kukinai kwa kile alichojaaliwa. Mke humpelekea kupendwa na mume wake. Pia mume anaondokana na wasiwasi anaamini chochote kile anachokipata akikipeleka kwa mkewe kinapokelewa bila ya shida.

“Zingatieni vyema haya tunayowambia, mumetuunganisha kuwa ndugu tafadhalini musije mukatufarakanisha tukaonana maadui, kwa sababu yenu umoja wetu muukuze na muulinde ili uendelee kudumu.”

Kauli ya nasaha ilipatikana kijiji cha Matale siku ya vyombo yaani baada ya ndoa kufungwa, kupitia baba mdogo wa biharusi alimueleza mtoto wake kuwa tayari ameshaunganisha udugu na kuwa wa moja baina yao. Tunategemea umoja na udugu huu muukuze na kuulinda ili usije ukavunjika. Jukumu la kila mmoja kuwa makini katika kujitahidi kuudumisha udugu huu ili uendelee kukua na kupatikana matunda yake. Kwani furaha yetu wazazi ni kuona watoto wetu wanaishi vizuri. Kwa hiyo, mke na mume muishi kwa salama mpaka wazae, wajukuu, watukuu hadi mmoja amzike mwenziwe.

Pia kauli za nasaha hazitolewi na wazazi peke yao, bali hutolewa na makungwi ambao hukaa nao maharusi katika kipindi cha fungate kwa kuwaelekeza mambo tafauti ambayo huleta tija kwao. Kungwi ni mtu anayemfundisha mwari wa kiume au wa kike kunga za nyumbani (TUKI, 2004). Mohamed na Mohamed (1998) wamefasili fungate ni siku saba za harusi. Pia TUKI (2004) inaelezea kuwa fungate ni muda wa siku saba baada ya harusi ambapo bwana na biarusi huutumia kwa mapumziko. Kwa hivyo, fungate ni kipindi ambacho maharusi hukaa ndani na kuhudumiwa. Aidha huwepo makungwi ambao ni watu wenye ujuzi huwapa maelekezo muhimu yanayohusiana na ndoa pamoja na utaratibu wote wa ndoa mfano kumsalimia mume, kutandika kitanda, kumuwekea chakula, kumpokea, kumsinga. Katika muktadha huu aghalabu biharusi na bwanaharusi hufundishwa kwa vitendo ili wazoweye mazingira hayo. Baadhi ya nasaha ambazo mtafiti alizipata kwa makungwi hizi zifuatazo:

“Sikiliza vyema haya tunayokunasihi, mume ana kazi, anahitaji malezi.”

Mtafiti akiwa katika kijiji cha Gongo Matale alimsaili kungwi juu ya kauli za nasaha anazowapa biharusi alieleeza kuwa humwambia mke anatakiwa amshughulikie mume wake kwa kumfanyia mambo mazuri yenye kumpendezesha. Inampasa mke aelewe mambo anayoyapenda mume wake ili azidi kuyadumisha katika kuyatekeleza. Pia humfahamisha mke ajue yale mambo yanayomkera mume wake na kuepukana nayo. Kutumia kauli nzuri zenye kumfurahisha mume wakati anapozungumza naye. Mke amuenzi na kumbembeleza mume wake kwa vile, ndiye mliwazaji wake. Pia mke si vibaya kumsaidia mume wake kwa kile ambacho ana uwezo nacho.

“Zingatia haya tunayokwambia, mume umsalimie asubuhi unapoamka na anaporudi safari zake ukimuona yule anakuja unyanyuke ukamsalimie.”

Kutokana na msingi wa nadharia ya uchambuzi makini wa matini unaosisitiza kuwa matini hufanyakazi kubwa katika kujenga na kupambanua itikadi za jamii katika matini hiyo. Mtafiti aliutumia kumsaili kungwi katika kijiji cha Chonga juu ya kauli nasaha ambazo huwapa maharusi kama ni itikadi ambazo hufanywa katika jamii yao. Kungwi alizungumza kuwa biharusi humuelekeza kumsalimia mume wake kwa maamkizi mazuri kama vile “sabalkheiri bwana” kwa wakati wa asubuhi na “msalkheiri bwana” kwa wakati wa jioni. Pia biharusi anaweza kumsalimia mume wake kwa kumwambia “chechei bwana” au “assalamu alaykumu bwana,” pamoja na kumpa mkono wakati wa kumsalimia kwani kukutana kwa viganja vyao mke na mume ni tiba. Inawezekana mmoja katika wawili hao akawa kuna jambo limempata au amekutana nalo la kumkasirisha lakini kupeana kwao mikono ikawa dawa ya

kuondoa tatizo hilo. Kwa hivyo, ni vizuri mke na mume kupeana mikono wakati wanaposalimiana.

“Sikiliza vizuri haya tunayokwambia, kitanda chako muda wote ukiweke katika hali nzuri.”

Mtafiti alipofanya usaili na kungwi katika kijiji cha Chuchuu Pujini, alieleza humnasihi biharusi, kwa kumwambia miongoni mwa mambo mazuri yanayompasa mke kuyafanya muda wote ni kutandika kitanda chake na kukiweka katika unadhifu. Tena atandike mitindo ya kila aina, wakati wote kitanda kiwe kinavutia pamoja na kutia manukato ya aina zote. Mume anapoingia ndani asitamani kutoka nje abakie ndani isipokuwa atoke kwa dharura maalumu. Mke anapoyadumisha mambo haya, mume anapomaliza harakati zake huharakisha kukimbilia nyumbani kutokana na mambo mazuri yaliyoko kwake ambayo mke anayatenda kwa mume wake. Pia humfanya mume kutokutumia muda mwingi nje, kukaa na watu wengine kuzungumza nao, isipokuwa mume pale anapopata dharura lakini akimaliza anarudi nyumbani mapema.

“Tunakunasihi, mke anatakiwa ajitahidi katika kumtuliza mume wake.”

Mtafiti alimshuhudia kungwi akimpa kauli za nasaha biharusi katika kijiji cha Chuchuu. Kungwi alimnasihi biharusi kwa kumwambia mke huwa na jukumu kubwa la kumtuliza mume katika mambo tafauti yakiwemo ya kiroho, kiakili na mengineyo. Mke anatakiwa kubuni mbinu zinazopelekea kumtuliza mume ili atulie pale anapokuwa na tatizo. Pia mke asishawishike na vishawishi anavyokutana navyo nje, kwake aone si lolote si chochote athamini zaidi ndoa yake.

“Jitahidi sana, umchunguze mume kumjua wakati huu yuko katika hali gani.”

Mtafiti alimshuhudia kungwi katika kijiji cha Matale akimnasihi biharusi kuwa ajitahidi kumsoma mume wake katika hali zote za furaha na huzuni. Kungwi alimwambia biharusi kuwa mumeo anaporudi katika harakati zake za kimaisha na akamfahamu kuwa hakurudi akiwa hali ya kawaida basi anapaswa kutaka kujua hali iliyomkabili na kumpa maliwazo alisahau tatizo alilonalo na kupelekea nafsi yake kutulia. Pia biharusi alinasihiwa kuepuka kutoa malalamiko pindi mume akiingia ndani tu hata haja pumzika.

“Zingatia vizuri tunayokunasihi, umuheshimu mumeo umuone ni mumeo wala usimdharau.”

Kauli ya nasaha hii ilipatikana mtafiti alipomsaili kungwi wa kijiji cha Gongo Matale. Kungwi alieleza kuwa humnasihi mke amuheshimu mume wake kwa kumuwekea heshima zote. Amuone kuwa ni mtu bora kwake kuliko wengine kwani ameona wengi amewaacha na amekuja kwake kumfariji ndipo chaguo lake liliporidhia. Kwa hiyo, mke athamini fursa adhimu aliyoipata. Kuna wengi ambao walikuwa wanaihitaji nafasi hii lakini hawakubahatika nayo na ikaangukia kwake. Hivyo, mke ajitahidi kuidhibiti na kuishikilia fursa hii ili isije ikamtoka. Pia mke hatakiwi kumkata mume wake jina akamwita kwa jina lake mfano Hamadi au Juma. Mke amwite mume wake kwa jina la kumpa heshima kama vile, bwana, mume wangu au jina lolote zuri ambalo mume analiridhia lenye kumfurahisha moyoni mwake wakati anapomwita.

“Sikiliza kwa makini haya tunayokwambia, mumeo anapokuja na mzigo unatakiwa umpokee.”

Mtafiti akiwa katika kijiji cha Chonga alimshuhudia kungwi akimpa kauli ya nasaha biharusi alimwambia mke anapomuona mume wake ana mzigo haraka amkimbilie na kumpokea. Kisha aukague mzigo huo kujua kilichomo kama muna kitu cha kuharibika akishughulikie wala asiupokee na kuuweka pembani bila kuwaangalia mpaka akaulizwa na mume wake. Kwa hiyo, mke asiwe na tabia hii inakuwa ni jeuri na mume anahisi kuwa anadharauliwa kitu ambacho si kizuri mtu kumfanyia mwenzake, ni vyema mke kuepukana nacho. Mke anapokuwa amejizowesha kawaida hii ya kumpokea mume wake. Mume anakuwa anafarajika na anajisikia kuwa anaheshimiwa. Hivyo, mke anajijengea tabia njema kwake na hupata upenzi mkubwa kwa mume wake.

Hivyo, kauli za nasaha za wakati wa ndoa hujikita katika kumfunza biharusi kutokuonesha mapambo yake nje ya nyumba yake, mume ndio kipaombele chake cha kwanza, kujiheshimu, kuomba msamaha anapokosea, kutokudai vitu ambavyo mume hana uwezo navyo, kutogombanisha familia ya mumewe, kutokasirika mume anapokasirika, kulinda heshima na nyumba ya mumewe

4.2.2 Kauli za Nasaha za Bwanaharusi

Katika upande wa bwanaharusi naye hupewa kauli za nasaha ambazo kwake ni ngao ya kuilinda ndoa yake. Kauli za nasaha hizi hupewa na wazazi, jamaa wengine wa familia, majirani pamoja na marafiki. Naye pia hupewa kauli za nasaha wakati wa posa na wakati wa ndoa

4.2.2.1 Kauli za Nasaha katika Posa

Kauli hizi hudhamiria kumuandaa kuwa mume bora. Kutokana na mabadiliko ya maisha utamaduni wa kuwaweka ndani maharusi pia umebadilika. Hivyo, kauli za nasaha hutolewa kwa bwanaharusi kila fursa inapopatikana. Kauli za nasaha katika kipindi hiki, zilizokusanywa katika utafiti huu ni:

"Mwanangu sikiliza kwa makini, nyumba ina mengi jitahidi utunze siri za nyumba yako."

Kauli ya nasaha ilipatikana kijiji cha Matale wakati mtafiti alipomsaili mtafitiwa alizungumza kuwa, moja ya kauli ya nasaha madhubuti ambayo alipewa ni utunzaji wa siri za nyumba. Nyumba ina mambo mengi, kuna kupata na kukosa, kuna yenye kufurahisha na kuchukiza. Pia mtafitiwa huyu alieleza kuwa aliambiwa pindipo kutatokea tatizo lolote la mivutano na mke wake, basi mivutano hiyo ibaki kuwa siri baina yao. Katu isitokee kuwaeleza marafiki zake au majirani juu ya mivutano iliyomo ndani. Pia mtafitiwa aliendelea kuzungumza kuwa alinasihiwa kwa kuambiwa kuwa adui mkubwa wa ndoa ni siri za ndani kuenea nje. Likifanyika hilo siyo mke tu ambaye atakataa kuendelea na ndoa hiyo, jamaa zake pia wanaungana naye. Hivyo basi, mambo ya ndani yaishie ndani hata kama kuna migogoro mikubwa wajitahidi watu wasijuwe. Kama imeshindikana hapana budi kuhudhurisha matatizo hayo kwa wazazi wa familia ya mke au mume ili kupata ufumbuzi muafaka.

"Jitahidi sana, usiwe mtu wa hasira kwani hasira hazileti mwelekeo nzuri katika ndoa."

Mtafiti akiwa katika sherehe ya harusi kijiji Mnazi Mmoja shehia ya Matale alimshuhudia baba mdogo wa bwanaharusi akimpa kauli ya nasaha mtoto wake

alimnasihi juu ya kuachana na tabia ya kukasirika ovyo. Kwa sababu hasira za kila mara humpunguzia mke hamu ya kuishi kwenye ndoa hiyo. Baadhi ya waliohojiwa wengine pia wamesema kuwa wapo baadhi ya waume ambao huwa na hasira zisizomalizika. Mume wakati mwengine huweza kukasirika bila ya sababu ya msingi. Hivyo, mume mtarajiwa alinasihiwa kwa kukanywa asiwe kama baadhi ya waume wengine wanapokuwa na hasira kuchukua hatua kali ikiwemo ile ya kuwapiga wake zao. Hatimaye hasara kumfika kama wasemavyo Waswahili kwamba 'Hasira hasara'. Hivyo kutokana na uzito wa kauli ya nasaha hii na namna vile itolewavyo, mara nyingi mume mtarajiwa huonyeka na pale tatizo linapojiri na likawa zito kwake kulitibu, huongozana hadi kwa wazazi wao ili kutafuta tiba ya tatizo hilo.

"Jitahidi sana, kushauriana na mkeo ndio mambo humea."

Mtafiti alimsaili mtafitiwa katika kijiji cha Jojo Matale juu kauli za nasaha ambazo amepewa, alieleza kuwa alinasihiwa awe na tabia ya kufanya mashauriano na mke wake katika mambo mengi. Hakuna kitu kizuri na kinachompendezesha mke kutoka kwa mume wake kama kushauriwa. Hivyo basi, mume ajitahidi kumshauri mke wake katika kila jambo alitendalo. Pia mtafitiwa aliendelea kueleza kuwa aliambiwa, katika kushauriana kwa mke na mume kunaweza kujitokeza mawazo mazuri juu ya jambo hilo ikawa ni njia moja ya kupata mafanikio. Kushauriana huleta baraka. Tabia hii ya kushauriana huweza kujengeka hata kwa kizazi chao wanachokizaa kurithi nyenendo njema za wazazi wao. Mambo tafauti katika nyumba yanafanikiwa kwa kuwepo mashauriano mema baina ya mke na mume. Ni vizuri wanandoa kushauriana katika harakati zao zote ili kupatikane ufanisi.

“Tunakunasihi, ujifunze mazuri yote ambayo mke anayo na umfunze mke mazuri yote ulio nayo ili kuweza kushirikiana katika kutekeleza mambo mazuri katika ndoa.”

Chanzo hiki cha taarifa kilipatikana katika kijiji cha Chonga, wakati mtafiti alipofanya mazungumzo na mtafitiwa juu ya kauli za nasaha alizopewa alieleza kuwa alinasihiwa kwamba, katika maisha ya ndoa mume na mke wanatakiwa kusomana tabia ili kila mmoja amfahamu mwenzake. Kufundishana mema yote ambayo kila mmoja ameyapata akiwa nyumbani kwao kupitia familia yake na jamii. Kutokana na kila mmoja amelelewa katika mazingira na jamii tafauti huwa na mambo mengi mazuri ambayo mwenzake hawezi kuyafahamu. Lakini munapo kuwa pamoja munaelimishana, kila mtu anapata kuelewa kile ambacho hakijui kutoka kwa mwenzake. Jambo hili husaidia kutengeneza mazingira mazuri katika ndoa. Pia huwa ni njia moja ya kuweza kurekebishana, kati ya mke na mume pale penye mapungufu.

“Sikiliza vyema haya unayoelezwa, jitahidi ufanye kazi sana ili uweze kutimiza mahitaji yako wala usimtegemee mke.”

Kauli ya nasaha hii ilipatikana kupitia baba mdogo wa bwanaharusi katika kijiji cha Mbuni Pujini alimnasihi mtoto wake kwa kumwambia mume anatakiwa ajitume sana ili aweza kukamilisha mahitaji ya nyumbani kwake. Mume ndiye mwenye jukukmu la kumshughulikia mke mahitaji yake yote wala asimtegemee mke kuwa ndiye ashughulikie mambo ya nyumba. Lakini mke anapokupa kitu kwa ridhaa yake, bila ya kumlazimisha huwa ni sadaka yake basi mume apokee na kutumia. Pia baba mdogo alimwambia bwanaharusi hana ruhusa ya kumtenza nguvu mke ili atoe kitu

chake kwa huduma za nyumba. Nakupa kauli ya nasaha hii kwa sababu katika jamii wapo baadhi ya waume ambao wanapooa majukumu yote ya nyumba humwachia mke. Jambo hili husababisha mke aone maisha ya ndoa ni machungu na hali ya kuwa ni neema pale yanapopatikana maelewano mema. Hivyo, mwanangu nakunasihi jiepushe na tabia hii ili kumpunguzia mke majukumu mazito.

"Jihadhari sana, usimruhusu mke kuwa na marafiki wengi na kutumia muda mwingi nje kwa kukaa na marafiki zake."

Mtafiti aliipata data hii kupitia dada wa bwanaharusi katika kijiji cha Matale alimnasihi ndugu yake kwa kumueleza juu kutokumuachia mke wake kuwa na marafiki hawa na wale ambao hawatampa mustakbali mwema na fikra nzuri. Kuna baadhi ya marafiki ni wema humuongoza katika mambo mema. Pia wapo marafiki wengine wabaya ambao wanaweza kumshawishi na maneno yakamuingia. Hatimaye mke akaingia katika mambo mabaya yakasababisha kukosekana maelewano mazuri kwa mume wake. Hivyo, bwanaharusi nakupa kauli ya nasaha hii ili kukuzindua hutakiwi utoe mwanya mkubwa kwa mke kuwa na kila aina ya marafiki. Jambo hili epukana nalo ili kuchelea kuja kumkosa mke kutokana na vishawishi vya nje vinavyozuka siku hadi siku.

"Tunakunasihi, unakwenda kumuoa mwanamke ana watani wake musije kwenda kwao akataniwa ukaja juu na kugombana na watu wake."

Hapa kabla ya kueleza makusudio ya kauli ya nasaha hii, ni vyema tuelewe utani ni nini? Utani ni tabia ya watu kufanyiana masihara kwa lengo la kuambiana kweli na kuimarisha uhusiano wao (BAKIZA 2010). Mtafiti akiwa eneo la utafiti katika kijiji cha Limani alimsaili mtafitiwa kutokana na kauli za nasaha ambazo amepewa

alieleza kuwa aliambiwa, mke huwa na watani wake. Watani hawa huwa wanatoka ndani ya familia moja ima wengine walisoma pamoja skuli, chuoni au madrasa. Hivyo basi, pindipo tumekwenda ukweni atambue kuwa lazima hili hutokea. Jambo hili lisikufanye kukasirika au kugombana au kupigana na watu kwa sababu ya kutaniwa mke wako na watani wake pale ambapo matani hayo hayakuchupa mipaka. Kwa hiyo, mume achukulie ni hali ya kawaida tu kwake wala asije akamfanyia mke mashaka wakati wakirudi nyumbani kwa sababu ya kutaniwa. Hata hivyo, mume awe mzingativu katika utani huo. Huenda mara nyengine ikawa mna ukweli wa jambo kwenye matani yenyewe.

4.2.2.2 Kauli za Nasaha katika Ndoa

Siku ya ndoa mume pia hupewa nasaha na wanafamilia, shekhe, kungwi, jamaa na hata marafiki. Wote hawa hubeba jukumu hilo ili kumsaidia bwanaharusi kujenga ndoa imara yenye mahaba na kuhurumiana. Kauli za nasaha zilizokusanywa katika utafiti huu zilikuwa:

"Jihadhari sana, linapotokea tatizo zifuatwe hatua mbalimbali za kufanya usuluhishi."

Mmoja miongoni mwa wanandoa kutoka katika kijiji cha Chonga wakati aliposailiwa na mtafiti alieleza kuwa kauli ya nasaha hii inamuelekeza mume anapokuwa na tatizo wakae pamoja na mke wake kutafuta njia faafu ya kuweza kuondosha tatizo hilo. Hutakiwa kila mmoja asikimbilie kwa jirani au rafiki kuanza kutaka ushauri wanaweza wakakupa shauri zuri. Wakati mwengine wanakupa fikra ambazo sio nzuri zikasababisha kuzidisha tatizo zaidi katika ndoa yenu. Pia mtafitiwa huyu aliendelea kueleza kuwa ni vyema mume na mke wajitahidi wenyewe

kutatua tatizo lao mpaka wahakikishe limekaa sawa. Pindipo limeshindikana, bora kulihudhurisha kwa wazazi, wakatoa msaada wa kulirekebisha. Kwa vile, wazazi ni wenye uoni wa mbali huenda likasawazishika.

“Tunakunasihini, mume na mke kuchokana katika maisha ya ndoa huwa ni uadui mkubwa.”

Kauli ya nasaha hii ilipatikana mtafiti alipomsaili mtafitiwa katika kijiji cha Limani alielezea kuwa katika maisha ya ndoa hujitokeza mambo mengi. Kuna mazuri na mabaya jambo la msingi mume na mke wavumiliane. Kutokana na kuwa yaliyomo katika maisha ya ndoa yanahitaji subira ya hali ya juu ili mume na mke waishi kwa salama na amani na kupelekea kudumu kwa ndoa yao. Pia aliendelea kusimulia kuwa si vyema mke au mume kuchokana kila mmoja akaona hana haja ya kuendelea na uhusiano wa kuwa pamoja katika maisha ya ndoa. Hivyo, hunasihiwa kupiga vita mawazo ya kuchokana katika nyoyo zao ili yasije sababisha kuharibu ndoa yao.

“Tunakunasihi uachane na mambo ya ujana umeshakuwa mtu mzima.”

Kauli ya nasaha hii ilitolewa na mama mzazi wa bwanaharusi katika kijiji cha Sebunyemi Matale, akimpa kauli ya nasaha bwanaharusi mtarajiwa alimnasihi mtoto wake kwa kumwambia, ameshakuwa mtu mzima atulizanishe akili zake vizuri kwa kuachana na masuala ya ujana kama kulewa na kwenda sehemu za starehe na kumuacha mke peke yake ndani. Kwa sababu endapo mambo haya akiyafanya, huenda ikawa sababu mojawapo ya kuharibikiwa na ndoa yako, kwani ujana ni nusu ya upumbavu kwa vile mtu anaweza kufanya mambo bila ya kujielewa. Hivyo basi, mama aliendelea kumnasihi mtoto wake kwa kumwambia ameingia katika ulimwengu mwengine ajichunge ili kuepuka kumkera mwenzake.

“Jihadhari sana, usiwadharau muliokuwa mukishirikiana pamoja kwa mambo tafauti kwa sababu ya kuoa.”

Mtafiti akiwa katika kijiji cha Melitano Chanjamjawiri alifanya usaili na mtafitiwa juu ya nasaha alizopewa, alizungumza kuwa alinasihiwa kwamba asivunje uhusiano wala mawasiliano na watu ambao alikuwa nao karibu hapo kabla ya ndoa. Watu hao akumbuke ameishi nao pamoja kwa muda mrefu na washauri wake wa kila jambo. Kukata uhusiano na mawasiliano huenda ikatokezea siku akawahitajia watu hao, nao wakamtenga. Hivyo, alinasihiwa kuwa siyo vyema kukaa nao mbali watu ambao mlikuwa pamoja kwa wema muda mrefu kwa sababu ya kuoa. Jambo la msingi ni kujipangilia vizuri kwa kukaa nao japo muda mdogo ili kuepuka jamii kukutizama kwa mtazamo mwengine.

“Sikiliza kwa makini haya tunayokunasihi, hapana haja ya kukusanya jamaa wa karibu kwa matatizo madogo madogo yanapotokea kati yako na mkeo.”

Kauli ya nasaha hii ilipatikana kutoka kwa kaka wa bwanaharusi katika kijiji cha Dodo Pujini alimnasihi ndugu yake kwa kumwambia, mume na mke wanatakiwa kuwa kitu kimoja wakati linapotokea tatizo. Mume awe ndio mahakama ya mke na mke naye awe ni mahakama ya mume katika kufanya usuluhishi wenye kufaa. Kwa hiyo, mume na mke wakae pamoja kwa ajili ya utatuzi wa tatizo linapotokezea mpaka wafikie hali ya maridhiano na kusameheana. Bila ya kushirikisha jamaa wa familia kuja kufanya suluhu. Mume na mke wakifuata utaratibu huu inapelekea kuinusuru ndoa kuingia katika matatizo na huishi salama bila ya migogoro.

Pia mtafiti alipata data kutoka kwa mashakhe kupitia usaili na wakati wa kufungisha ndoa. Siku ya ndoa kufungwa ndio kilele cha siku ya harusi ambayo hukutanishwa wanandoa hao na kuwa tayari wameshahalalishwa kuwa mke na mume. Katika jamii ya Wapemba, ndoa nyingi hufungwa katika eneo la misikitini. Endapo ikitokea kuwa mahala hapo msikiti wake upo mbali, ndipo ndoa hiyo inapofungwa nyumbani kwao biharusi. Watu hukaa ukumbini (sebuleni) au uwanjani. Mara nyingi wale wageni waliohudhuria yaani, wageni waliokuja na bwana harusi, wao hutakiwa wakae ndani wakiwa pamoja na wenyeji wachache. Bwanaharusi hupewa kauli za nasaha hizi hadharani mbele ya watu wote ambao wamekusanyika shughulini hapo. Tofauti na upewaji wa kauli za nasaha wa biharusi ambao hupewa sehemu faragha pakiwa na watu wachache. Baadhi ya kauli za nasaha ambazo mtafiti alizipata kupitia kwa mashekhe ni hizi zifuatazo:

“Jitahidi sana, uchunge amana hii uliyopewa kwa kukaa naye mke kwa wema na hatupendi litokee jambo la kuachana lakini likitokea basi mtokane kwa wema.”

Kauli ya nasaha hii ilipatikana kwa shekhe wa kijiji cha Chanjamjawiri wakati aliposailiwa na mtafiti juu ya kauli za nasaha anazowapa maharusi. Shakhe alizungumza kuwa humnasihi mume kuishi na mke wake vizuri. Mume anatakiwa afahamu kuwa ameshabeba jukumu na kuchukua ahadi kwa Mwenyezi Mungu na mbele ya mashahidi pamoja na watu wengine ambao wamehudhuria katika ufungaji wa ndoa hiyo. Kwa hiyo, shekhe humnasihi mume ajitahidi kusimamia dhamana hii ya kuishi kwa wema na mke wake. Halikadhalika shekhe alieleza humwambia mume kuwa kwenda kinyume na ahadi hii ni kujiingiza katika makosa. Jambo jengine muhimu kwenye kauli ya nasaha hii, humnasihi bwanaharusi kuwa afanye bidii ya

kuepukana na suala la talaka kwa kuandaa misingi mizuri katika ndoa. Jambo la kupeana talaka si jema isipokuwa pale ambapo hapana budi.

“Tunakunasihi, uwe na upendo kwa mke wako.”

Mtafiti akiwa uwandani alimsaili shekhe wa kijiji cha Kichanjaani Pujini kutokana na kauli za nasaha anazowapa maharusi, alieleza kuwa ingawa kauli ya nasaha hii hupewa bwanaharusi, lakini ilivyo huwalenga wanandoa wote wawili mke na mume. Makusudio ya kauli ya nasaha hii ni kumuaidhi bwanaharusi kuwa katika maisha ya ndoa, ni muhimu kwa mume na mke kuwa na mapenzi ya kweli kila mmoja kwa mwenzake. Jambo hili husababisha ndoa kudumu. Matokeo ya jambo hilo huwakinga mume na mke katika kuathiriwa na fitina za maadui wa nje kutokana na mapenzi yaliyojengeka katika nyoyo zao. Pia ndoa inakuwa na baraka na furaha siku zote kutokana na mume na mke kuwa na mapenzi ya kweli baina yao. Lakini mapenzi yanapokosekana kwa mke na mume au mmoja miongoni mwa wawili hao, huenda ndoa hiyo ikaleta masahibu kadha wa kadhaa. Nadharia ya uchambuzi makini wa matini iliyotumika katika kuchambua kauli za nasaha katika harusi za Wapemba inaonesha kwamba, maisha ya wanandoa yanahitaji mapenzi ya kweli. Jambo muhimu ni kutumia busara na hekima kwa mke na mume wala wasiwe na pupa na vishindo.

“Sikiliza vyema haya tunayokunasihi, mwanamke kaumbwa kwa ubavu uliopinda, ukiamua kuunyoosha unaweza kuukata, ukiamua kustarehe nao, basi starehe nao hali ya kuwa umepinda na ukiamua kuukata basi hiyo ni talaka.”

Mtafiti alifanya mazungumzo na shekhe wa kijiji cha Limani juu kauli ya nasaha anazowapa maharusi. Mtafiti alieleza kuwa kauli ya nasaha hii huitoa kwa lengo la kumfahamisha bwanaharusi kwamba mke ana mapungufu tafauti ya tabia kimaumbile. Hivyo basi, shekhe alimnasihi bwanaharusi kutumia hekima na busara katika kumuongoza mke kwa kumfahamisha na kumuelekeza taratibu taratibu mpaka afikie makusudio ili kupatikane mafanikio mema ya ndoa. Pia mume alinasihiwa kwamba mke si lazima kutekeleza kila analomuagiza papo hapo kwani kwa desturi ya baadhi ya wanawake hatoweza kufanikiwa, hutaka ajionesha kuwa naye anayo maamuzi kama binadamu wengine.

"Zingatia vizuri haya tunayokunasihi, umshughulikie mke kwa kumpa chakula, mavazi na makazi kwa kadiri ya uwezo wako."

Kauli ya nasaha ilipatikana wakati shekhe akifungisha ndoa katika kijiji cha Matale. Shekhe alimueleza bwanaharusi kuwa ni jukumu lake kumpatia mahitaji ya msingi mke wake kwa mujibu wa uwezo wake. Ikiwa mume uwezo wake wa ruhusu, amshughulikie mke kwa kumpatia kila anachohitajia, pasi kufanya ubakhili na kumsumbulia. Hata hivyo, mtafiti amebaini mke kuwa pindipo uwezo wa mume wake ni dhaifu, basi avumilie. Uvumilivu ni muhimu na mara nyingi huleta tija katika siku zijazo. Hivyo, mke hutakiwa asifanye mashaka huenda siku za mbele mambo yakawa mazuri.

"Tunakunasihi umshughulikie mke kwa kumpatia matibabu."

Mtafiti alipokuwa kijiji cha Limani alimsaili shekhe kutokana na kauli za nasaha anazowapa maharusi. Shekhe alieleza humnasihi bwanaharusi kwamba ni wajibu wake inapotokezea mke kuwa mgonjwa amshughulikie kwa kumtibu mpaka apowe

maradhi aliyonayo. Mume haimstahikii kukwepa jukumu hilo akawaachia wakwe zake akaona ndiyo wanaohusika kumshughulikia mtoto wao. Kwa vile mume alipomchukua mke kwao alichukua ahadi ya kumuhudumia kwa kila jambo. Pindipo hali yake mume hairuhusu, hapana tatizo kuomba msaada kwa wakwe zake ili wamsaidie.

"Tunakunasihi, haipendezi kwa muumini mwanamme kutengana na muumini mwenzake mwanamke kwa sababu tu amekukera. Wanawake wanapika vyakula vyetu, wanafua nguo zetu na wanalea watoto wetu. Inapotokezea mke amekukera, basi isiwe wewe (mume) kushikilia baya alilokutendea ilhali yapo mazuri mengi aliyoyafanya juu yako. Madhali kosa alilokufanyia halivunji heshima ya dini na heshima yako msamehe."

Shekhe alipokuwa akifungisha ndoa katika kijiji cha Limani, alimnasihi bwanaharusi kwa kumwambia, inapotokea mke wake amefanya jambo ambalo halikumfurahisha asichukulie hasira tu moja kwa moja, ikapelekea kuharibu yale mazuri mengi ambayo mke ameyafanya kwa mume wake. Isipokuwa akumbuke jema jengine analolipenda lenye kumfurahisha na kumvutia zaidi ambalo mke wake amemfanyia na kusahau lile baya. Kwa hiyo, mume alinasihiwa kuwa isiwe anamuangalia mke wake kwa upande wa makosa tu na kumuangushia lawama hizi na zile pamoja na kumchukulia hatua. Bali mume aangalie pia mazuri mengi ambayo mke amemfanyia kadri ya siku zinavyopita ili waendelee kuishi pamoja kwa furaha na amani.

"Sikiliza kwa makini haya tunayokunasihi, mume anatakiwa aoneshe mapenzi zaidi katika familia ya mke wala asidharau familia yake."

Kauli ya nasaha hii ilipatikana katika kijiji cha Matuleni katika shehia Matale wakati shekhe akifungisha ndoa. Shekhe alimnasihi bwanaharusi kuwa aoneshe mapenzi kwa familia ya mke ili wanafamilia waone kuwa wameongeza mtu mwengine mwenye kuwajali katika ukoo wao. Hata hivyo, bwanaharusi alinasihiwa kuwa asije akaondosha mapenzi kwa familia yake kwa sababu ya kuoa na ikawa mapenzi yote yameegemea upande wa familia ya mke. Mume akumbuke kwamba wazazi nao wana sehemu kubwa kwake ya kuonesha upendo kwao.

“Jihadhari sana, wala isiwe tena limetokezea kosa mbio unakimbilia maskani kuhadithia. Mtu wa maskani mwenyewe hana mke au pengine yule mke wako pia yeye anamtaka, anatamani umuwache amuowe yeye. Baada ya muda anakupa ushauri ambao ni mbovu hauna faida unamuacha mke wako anamuoa yeye. Baadae utasikia anamwambia rafiki yangu sikutegemea kama utanifanyia haya amesha muoa yeye zamani mke wako.”

Kauli ya nasaha ilipatikana katika kijiji cha limani wakati shekhe alipokuwa akifungisha ndoa. Shekhe alimfahamisha mume kuwa linapotokea tatizo baina yake na mke wake asikimbilie katika eneo ambalo halistahiki kwenda kutoa kero zake, kwani kufanya hivyo huhatarisha usalama wa ndoa yake. Bali mume anatakiwa kukaa pamoja na mke wake, kufanya utatuzi wa tatizo unaofaa ili kuepusha kujulikana tatizo lao na watu wengine. Pia marafiki anaowaelezea kuna hatari ya kuja kumvunjia nyumba yake yaani kumpokonya mke wake na kumuoa mmoja miongoni mwao.

Pia kauli za nasaha hutolewa na wazazi pamoja na jamaa wengine siku ya vyombo ambapo hufanya makabidhiano ya ulezi baina ya familia ya bwanaharusi na biharusi.

Baadhi ya kauli za nasaha ambazo mtafiti alizikusanya siku ya vyombo ambazo alipewa bwanaharusi ni hizi:

"Jitahidi sana, baba sifa za mkeo zibakie ndani wala usizieneze kwa kila mtu akazijua."

Kauli ya nasaha hii ilitolewa na baba mdogo wa biharusi katika kijiji cha Njia ya Kidongo Chanjamjawiri siku ya kupeleka vyombo alimueleza mkwe wake (bwanaharusi) asipende kuhadithia mambo ya mke wake kwa watu wengine. Isipokuwa abakie nayo mwenyewe katika moyo wake kwa yale mazuri na hata mapungufu kwani hakuna kiumbe ambaye ni mkamilifu. Kila mmoja ana mazuri yake na kasoro zake kwa mwenzake la msingi ni kuvumialiana. Maisha ya ndoa yanahitaji subira kubwa ndio wanandoa wanaweza kuishi pamoja.

"Nakuusia na utumiaji wa talaka za kutega au kutundika sio nzuri."

Kauli ya nasaha hii alipewa bwanaharusi na baba mdogo wa biharusi wakati wa makabidhiano (siku ya vyombo) katika kijiji cha Kipapo. Baba wa biharusi alimtahadharisha mkwe wake juu ya jambo la talaka za kupachikiza. Baadhi ya waume hupenda sana kutumia talaka hizi kwa wake zao bila kufikiria madhara yake hapo baadae. Mke anaweza kukatazwa jambo na mume wake kwa kumwambia akifanya jambo hili ndio talaka yake. Mke naye anaweza akalifanya kwa makusudi bila hata kujali kwa kuangalia athari yake. Mwisho, mke anaachika kwa jambo ambalo halina msingi na huku bado mume anamtaka. Kwa hiyo, mume ajiepushe na jambo hili si zuri linapelekea ndoa kuingia katika matatizo ambayo yanaweza kuepukika.

"Jihadhari sana, usimdanganye mkeo kwa kitu usichokuwa na uwezo nacho, unaweza kusababisha matatizo katika ndoa yako."

Kauli ya nasaha hii ilitolewa na baba mdogo wa biharusi katika kijiji cha Kipapo Chonga. Baba alimuelekeza bwanaharusi asimuahidi mke wake mambo makubwa asiyo yamiliki wakati kipato chake ni cha chini kuliko yale ambayo ameahidi. Mke naye huingia tamaa ya kupatiwa vitu hivyo. Kila siku, mke anasubiria lakini haoni kuletewa na mume wake. Baadaye, mke huzusha machafuko na kuanza kukosekana amani katika nyumba yao. Hivyo, mume ni vyema kutoa ahadi ambayo anaweza kuitekeleza ili kuepusha kutokea kwa migogoro katika ndoa. Mume akifanya hivyo kunapelekea usalama wa ndoa na mke naye aelewe kuwa huo ndio uwezo wa mume wake.

"Zingatia haya tunayokwambia, ukitaka kujua utamu wa ndoa uwapende wakwe zako. Hawa ndio silaha katika kuilinda ndoa yako"

Mtafiti alishuhudia kauli ya nasaha iliyotolewa na mjomba wa bwanaharusi katika kijiji cha Mtondooni shehia ya Chonga. Mjomba alimnasihi mtoto wake ashikamane na familia ya mke hasa wazazi ambao ndio nguzo imara katika kumtengenezea mazingira mazuri ya ndoa yake na kuifanya idumu. Pia mke anapopendewa wazazi wake na mume, huwa anatulia nafsi yake na huzidi kukupenda sana. Mjomba aliendelea kuzungumza mume anapojenga mapenzi mazuri kwa wakwe zake inapelekea wakwe nao wakupende, wakuthamini na wakujali. Pia mume linaweza likatokea tatizo kati yako na mkeo na mke akapeleka kesi kwao. Wazazi wakamkatalia kuwa hawezi mumeo kukufanyia hivi, kutokana kuwa amewaweka vizuri. La akiona mume ameshapata mke akawa kwao wakwe huna haja nao tena,

basi huwa anajivunjia katika ndoa yake kwani wazazi ndio ngao muhimu katika kuiyengaenga ndoa yake.

“Nakutanabahisha na simu, mulipokuwa hamjaoana mulikuwa na marafiki wa kike na kiume mukiwasiliana. Kuanzia sasa kila mmoja, awe na namba za simu za watu wa familia yake na kila mtu azifahamu namba za mwenzake.”

Nasaha hii ilitolewa na mama mdogo wa bwanaharusi katika kijiji cha Chanjaani Matale, aliwatahadharisha bwanaharusi na biharusi juu ya suala la matumizi ya simu na kila mmoja kuwa makini na simu yake. Mume awafahamu vizuri watu wa familia ya mke na mke naye awaelewe vyema watu wa familia ya mume ili kuepusha kupigwa simu ya mmoja kati yenu akawa mtu hamfahamu ikapelekea kukosekana amani katika nyumba. Mama mdogo aliendelea kuwanasihi maharusi kwa kuwaambia baadhi ya wanandoa hutumia simu vizuri na wengine hutumia vibaya. Ni vyema mume na mke kuwa wawazi katika matumizi ya simu ili kujenga uaminifu kila mmoja kwa mwenzake utumiaji wa simu. Tukizingatia ya kwamba, katika ulimwengu wa sasa matumizi ya simu yamekuwa kwa kiwango kikubwa. Watu hutumia mitandao ya kijamii katika shughuli tafauti.

“Zingatieni vyema haya tunayowambia, mumetupa ulezi tumeupokea kwa mikono miwili kwa lolote litakalotokea. Ikiwa ulezi umelelewa na kuiga tabia kama ulizotoka nazo kwao, ulezi huu utakuwa ni wenye ufanisi, lakini ikiwa utaiga tabia nyengine, hapa ukaona una mamlaka yake hahitaji tena kulelewa, ulezi huu utafanya mashaka kidogo kwani kizazi chetu cha sasa muna kijua hakitaki kuelekezwa. Kwa hivyo, awe kama kizazi cha zamani ametoka kwenye mikono ya wazee na ameingia

katika mikono ya wazee wengine. Pia tuko pamoja kwa lolote linalotokea la heri au shari.”

Kauli ya nasaha hii ilitolewa na mjomba wa bwanaharusi baada ya kukabidhiwa ulezi na familia ya biharusi. Mjomba alikiri kwa niaba ya wenzake kuwa wameupokea ulezi na kuulea kwa kumsimamia katika mambo yote mema na kumkataza kwa yale mabaya. Endapo jukumu hili hawakulitekeleza wazazi pamoja na mume huingia makosani. Kwa hiyo, Mke aliambiwa na wazazi wake akubali kulelewa awaone wakwe zake kama wazazi wake. Pia wazazi wa biharusi walieleza panapotokea ugumu katika ulezi huo ni vyema kuwaarifu ili kusaidiana katika kuitengeneza ndoa.

Pia kauli za nasaha huwa makungwi hawazitoi kwa biharusi tu bali humpa na bwanaharusi kipindi cha harusi ambacho hukaa nao pamoja. Baadhi ya kauli za nasaha mtafiti alizozipata kupitia makungwi ambazo humnasihi bwanaharusi ni hizi:

“Tunakunasihi, mke ni mkeo, ndio mwenzio usimfanyie jeuri wala dharau.”

Mtafiti alipata taarifa hii ya kauli ya nasaha kutoka kwa kungwi wa kijiji cha Gongo Matale, wakati alipomsaili juu kauli za nasaha anazowapa maharusi. Kungwi alieleza kuwa humnasihi bwanaharusi kuishi vizuri na mke wake kwa kumlea katika malezi mazuri. Amthamini na kumuona kuwa ni mtu muhimu kwake na mwenzake wa kushauriana na kusaidiana katika maisha. Pia mume ampe maneno mazuri mke wake yenye kumfurahisha na kumliwaza ili atulie moyo wake na aone ndoa ni faraja kubwa kwake.

"Sikiliza vyema haya tunayokunasihi, mke anahitaji matunzo."

Taarifa hii ilipatikana mtafiti alipomshuhudia kungwi akitoa kauli ya nasaha kwa bwanaharusi katika kijiji cha Chuchuu. Kungwi alimnasihi bwanaharusi kwa kumsisitiza juu ya kumtunza mke wake vizuri. Kungwi alimwambia mume, mke ni sawa na ua, linapotunzwa vyema humea na kustawi vizuri lakini linapokosa kutunzwa vyema hunyauka. Hivyo hivyo ni sawa na mke anapotunzwa vizuri anakuwa mzuri mwenye kupendeza na kuvutia na anapokuwa hana matunzo, uzuri wake hupotea. Kwa hivyo, mume amtunze vizuri mke wake ili atulie katika nyumba yake asihangaike.

"Jihadhari mno, munapokosana na mkeo musigombane uwanjani."

Mtafiti aliomba ruhusa kwa kungwi katika kijiji cha Chanjaani Matale ili kushuhudia kauli za nasaha anazowapa maharusi. Kungwi alimnasihi mume kwa kumwambia mume na mke wanapokuwa na tatizo wanatakiwa kutumia njia iliyo bora yenye kuleta ufanisi katika kutatua tatizo hilo. Wala isiwe kila mmoja kusimama hadharani na kuanza kutoleana aibu zenu tafauti, ikapelekea jamii kujua mambo ya ndani ambayo haipendezi kutambuliwa na watu wengine. Maisha ya ndoa huwa na mambo mengi muliyofanyiana, kuna mema na mabaya. Jambo hili halileti picha nzuri kwa wanandoa, hasa ukizingatia mumeshakuwa kitu kimoja kwa kuunganisha udugu baina yenu.

Kwa maana hiyo bwanaharusi ananasihiwa kutokimbilia kutoa talaka, kutotoa aibu za mkewe, wasizozane hadharani, asimruhusu mkewe kuwa na mashoga wengi, awatambue watani wa mkewe, wasikimbilie kupeleka kesi kwao, asimtegemee mke

kutimiza mahitaji ya nyumbani yaani chakula, mavazi na malazi, amtunze vizuri mkewe, amuhukumu mkewe kutokana na mazuri yake na si mabaya yake.

4.3 Kauli za Nasaha Zinavyojenga Uhusiano wa Wanandoa

Lengo hili lilichambuliwa kwa kuongozwa na msingi wa pili wa nadharia ya uchambuzi makini wa matini ambao ni mahusiano ya nguvu na mamlaka katika jamii hujengwa katika mfumo wa uhusiano uliopo katika utumizi wa lugha ndani ya matini. Mtafiti kupitia lengo la kwanza la utafiti ambalo ni kuainisha kauli za nasaha anazopewa biharusi na bwanaharusi kwa mujibu wa utamaduni wa Wapemba. Mtafiti aligundua kuwa kauli za nasaha zinajenga uhusiano baina ya biharusi na bwanaharusi katika maisha ya ndoa. Uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha husaidia kutengeneza mazingira mema ya ndoa kwa kuishi salama baina ya mke na mume. Baada ya mtafiti alipokusanya data zilizopatikana kwa watafitiwa zilithibitisha kuwa kuna uhusiano wa kauli za nasaha anazopewa bwanaharusi na biharusi uliodhahiri katika jamii ya Wapemba. Miongoni mwa uhusiano uliopatikana kutokana na kauli za nasaha ni: wanandoa huishi kwa furaha katika maisha ya ndoa, wanandoa huleana katika misingi mema, mume na mke kuwa na mashirikiano mema, wanandoa hujengeana heshima, wanandoa huishi kwa kuhurumiana, wanandoa huepukana na migogoro katika ndoa, wanandoa huwa wavumilivu katika ndoa, wanandoa hupata utulivu katika ndoa, wanandoa huongezeka kipato (uchumi), mke na mume huishi kwa kushauriana, wanandoa hupata ukumbusho, wanandoa hubadilika kimwenendo, wanandoa kuwa na ujasiri, wanandoa hupata matayarisho mazu**ri** wanapoingia katika ndoa, wanandoa hufahamu wajibu wao.

4.3.1 Wanandoa Huishi kwa Furaha katika Maisha ya Ndoa

Mwanandoa mmoja wa kike kutoka kijiji cha Matale alieleza kuwa, moja ya uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha kwa biharusi na bwanaharusi, katika jamii ya Wapemba ni kupatikana furaha ya ndoa baina ya mke na mume na hata kwa familia zao. Kutokana wanandoa hao hupata kauli za nasaha nyingi mno zinazohusu maisha ya ndoa. Basi, wanandoa huishi kwa furaha na upendo mkubwa katika ndoa. Hata, panapotokea mgongano kati ya wanandoa hao, mmoja huweza kukumbuka kauli za nasaha walizopewa ya ustahamilivu hurudi matawi ya chini na kuendelea na maisha ya ndoa yao kwa furaha na amani.

4.3.2 Wanandoa Huleana katika Misingi Mema

Mtafitiwa kutoka kijiji cha Gereji Chanjamjawiri, alieleza kauli za nasaha ambazo hupewa biharusi na bwanaharusi hujenga uhusiano wa kuleana katika misingi mema katika maisha ya ndoa. Mfano mke alinasihiwa kwa kuambiwa mume anakazi anahitaji malezi. Mke anafahamishwa kuwa amshughulikie mume wake vizuri kwa kumtimizia mahitaji anayostahiki kupatiwa kutoka kwake. Pia mume alinasihiwa kwa kuelezwa kuwa mke anahitaji matunzo. Hapa mume aliambiwa kuwa mke ni sawa na ua, anapolitunza vizuri hustawi na kuvutia na asipolishughulikia hupoteza haiba yake. Hii ina maana kwamba mume anatakiwa amlee mke wake kwa kumtunza vyema. Kauli za nasaha hizi zina uhusiano kwani zote zinasisitiza juu ya kuleana vizuri baina ya mke na mume katika maisha ya ndoa.

4.3.3 Mume na Mke kuwa na Mashirikiano Mema

Mtafitiwa kutoka kjiji cha Matale alieleza kuwa mume na mke wanapopata kauli za nasaha wanapoingia katika maisha ya ndoa, hupelekea kuwa na mashirikiano ya hali ya juu katika harakati zao zote. Mfano mke alinasihiwa ‘awatunze wazazi wa mume pamoja na jamaa zake.’ Pia mume alinasihiwa ‘akitaka kujua utamu wa ndoa uwapende wakwe zako, hawa ndio silaha katika kuilinda ndoa yako.’ Kauli za nasaha hizi zinajenga uhusiano kwani zinawasisitiza mke na mume kujenga mashirikiano mazuri. Mke ashirikiane na familia ya mume katika mambo yote ya harusi, maziko, ugonjwa na matembezi ya kawaida kwani familia ya mume, ndugu yao anapooa huona kuwa wameongeza mtu mwengine katika familia yao. Halikadhalika mume naye ashirikiane na familia ya mke katika mambo tafauti kwa vile naye ni sehemu ya familia ya mke. Jambo hili huzifanya familia hizi kuunganika na kuwa kitu kimoja.

4.3.4 Wanandoa Hujengeana Heshima

Mtafiti alipata taarifa hii ya kauli ya nasaha kutoka kwa mtafitiwa wa Kijiji cha Chuchuu Pujini alieleza kuwa kupitia kauli za nasaha ambazo hupewa biharusi na bwanaharusi hupelekea kujengeana heshima. Mfano mke alinasihiwa kuwa ‘umuheshimu mumeo umuone ni mumeo wala usimdharau.’ Mume naye alinasihiwa kwa kuambiwa ‘mke ni mkeo, ndio mwenzio usimfanyie jeuri wala dharau.’ Kauli za nasaha hizi zinajenga uhusiano zote zinawahimiza mume na mke juu ya kuheshimiana katika maisha ya ndoa.

4.3.5 Wanandoa Huishi kwa Kuhurumiana

Mtafitiwa kutoka kijiji cha Njia ya Shungi Chanjamjawiri, alizungumza kuwa miongoni uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha ni kwamba wote wawili mke na mume hunasihiwa juu ya kuhurumiana. Mke amuhurumie mume wake. Pia mume awe na huruma kwa mke wake. Kutokana huruma hizo hujenga upendo kwa wanandoa hao. Mume na mke wanapoishi kwa kufuata msingi huu hupatikana ufanisi katika ndoa. Mume na mke hupelekea kuishi maisha mema ya kuthaminiana, kupendana, kujaliana kutokana na kuhurumiana kwao. Halikadhalika, wanandoa hupelekea kila mmoja kuwa karibu na mwenzake pamoja na kusaidiana wakati wa raha na matatizo. Wanandoa wanapolidumisha hili, ndoa hupata baraka pamoja na kudumu kwa ndoa yao. Jambo hili hupatikana kupitia uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha wanazopewa.

4.3.6 Wanandoa Huepukana na Migogoro katika Ndoa

Mwanandoa mmoja wa kiume kutoka kijiji cha Chonga alieleza kuwa kutokana na wanandoa hulelewa na kukulia katika mazingira ya utumiaji wa kauli za nasaha. Kauli za nasaha hizi, huwaingia vichwani mwao pamoja na kuziendeleza katika kila hatua wanayoipitia katika maisha yao. Mfano mume alinasihiwa kujiepusha na hasira na mke alinasihiwa kujiepusha na tabia ya kununa. Kauli ya nasaha hii imesaidia kujenga uhusiano kwa wanandoa katika kuishi salama bila ya migogoro kama ugomvi, chuki, fitina kati ya mume na mke na hata jamii zao zilizowazunguka kwa ujumla. Pia wanandoa huzitumia kauli za nasaha kama muongozo kwao ambapo uhusiano huu husaidia kujenga uwimara na hupelekea kudumu kwa ndoa na kuepukana na matatizo kutokana na kuzitilia umuhimu kauli za nasaha walizopewa.

4.3.7 Wanandoa Huwa Wavumilivu katika Ndoa

Katika maisha ya ndoa hufungamana na mambo mengi kuna yenye kufurahisha na kuchukiza. Mtafitiwa kutoka kijiji cha Kipapo alieleza kuwa mume na mke hali zote hizi wanaweza kukumbana nazo katika maisha ya ndoa, lakini wawe wavumilivu. Mfano mume alinasihiwa kuwa ‘hapana haja ya kukusanya jamaa wa karibu kwa matatizo matatizo madogo madogo yanapotokea kati yako na mkeo.’ Hapa mume anafahamishwa awe mvumilivu isiwe tatizo dogo likitokea anakimbilia kwa wakwe kuweka vikao, jambo hili si jema. Isipokuwa mume na mke wasuluhishane wenyewe. Pia mke amenasihiwa ‘asimdai mume kitu asichokuwa na uwezo nacho, aridhike na anachopewa’. Hapa ananasihiwa mke naye kuwa na tabia ya uvumilivu kwa kupokea kile ambacho ndio uwezo wa mume. Hivyo kauli za nasaha hizi zina uhusiano kwani zinasisitiza mume na mke kuvumiliana katika maisha yao ya ndoa.

4.3.8 Wanandoa Hupata Utulivu katika Ndoa

Mtafitiwa kutoka kijiji cha Melinne Chanjamjawiri alieleza miongoni mwa mambo ambayo hujenga ndoa ni kupatikana kwa utulivu kwa mke na mume. Ndoa inapokuwa na utulivu hupelekea mke na mume, kutulia nafsi zao na kuishi maisha mema. Wala si rahisi kuweza kuingia fitina za maadui dhidi ya ndoa yao. Kitu hiki hupatikana kutokana na zile kauli za nasaha wanazopewa kipindi wanapoingia katika ndoa. Mfano mke hunasihiwa kuwa awe mwema kwa mume wake na mume hunasihiwa juu ya kuwa na upendo kwa mke wake. Kauli za nasaha hizi zina uhusiano, kutokana kuwa mke akiwa mwema na mume anapokuwa na upendo, mambo haya hupelekea kwao kupatikana utulivu katika maisha ya ndoa. Bila ya kuwepo kwa utulivu ndoa huyumba.

4.3.9 Wanandoa Huongezeka Kipato (Uchumi)

Mtafitiwa kutoka katiak kijiji cha Dodo Pujini alieleza kuwa, katika siku za mwanzo mke na mume wanapooana huwa katika hali duni ya maisha kutokana kuwa ndio kwanza wanaanza maisha ingawa wengine huwa na uwezo nzuri wa kimaisha. Baada ya muda mke na mume maisha yao huanza kubadilika kidogo kidogo. Hatimaye, wanandoa hawa hali zao hunyanyuka kimaisha na kuwa nzuri hupelekea kumiliki vitu tafauti ambapo hapo awali hawakuwa navyo. Wanandoa wale ambao hali zao za maisha ni nzuri huzidi kiuchumi. Hii inatokana namna kauli za nasaha zinavyojenga uhusiano baina ya mke na mume. Mfano mume hunasihiwa kupambana katika kufanyakazi wala asimtegemee mke na mke hunasihiwa kutunza mali. Hivyo, kauli za nasaha hizi zinajenga uhusiano kutokana kuwa mume huhimizwa kutafuta na mke anatunza kile kinachopatikana.

4.3.10 Mke na Mume Huishi kwa Kushauriana

Mtafitiwa kutoka kijijij cha Matale, alieleza kuwa kauli za nasaha hujenga uhusiano kati ya mke na mume huwafanya waishi vizuri kwa kushauriana katika maamuzi yao yote. Mume na mke huwa kama kanuni kwao kuwa mtu hawezi kufanya jambo lolote kwa kutoa maamuzi ya pekee bila ya kumshirikisha mwenzake. Mfano mke hunasihiwa juu ya kuwa ‘muwazi kwa mume wake,’ kwa maana hiyo jambo lolote analolifanya mke huwa anamshauri mume wake na hatofanya siri. Pia mume naye hunasihiwa ‘kushauriana na mke wake ndio mambo humea.’ Kutokana na msingi wa pili wa nadharia ya uchambuzi makini wa matini ambao ni mahusiano ya nguvu na mamlaka katika jamii hujengwa katika mfumo wa uhusiano uliopo ndani ya matini. Hapa tunaona kauli za nasaha hizi namna zinavyojenga uhusiano katika kuhimiza

mke na mume kuwa na mashiuriano katika maisha yao ya ndoa. Hivyo, mume na mke ni vyema kuishi kwa kushauriana kwani kushauriana hujenga upendo na uaminifu katika ndoa.

4.3.11 Wanandoa Hupata Ukumbusho

Mtafitiwa kutoka kijiji cha Kichanjaani alizungumza kuwa kauli za nasaha ni ukumbusho tosha kwa wanandoa. Mume na mke wanapozikumbuka kauli za nasaha ambazo walipewa hupelekea kuwa watiifu na kurudi matawi ya chini kabla ya kufanya maamuzi magumu. Kutokana msingi wa pili wa nadharia ya uchambuzi makini wa matini unaonesha mahusiano ya nguvu na mamlaka katika jamii hujengwa katika mfumo wa uhusiano uliopo katika utumizi wa lugha ndani ya matini. Hivyo, kauli za nasaha zinazotolewa katika harusi za Wapemba hujenga uhusiano baina ya mke na mume katika jamii hiyo. Mfano mke alinasihiwa asitoke bila ya ruhusa ya mume wake. Jambo hili humpa ukumbusho mke anapopata safari, jambo la mwanzo akimbilie kuomba ruhusa kwa mume wake. Pia mume alinasihiwa kukaa na mke kwa wema. Hapa mume hupata ukumbusho pale anapoazimia kumfanyia mke wake mambo mabaya hupelekea kuachana nayo. Kwa hivyo, kauli za nasaha hupelekea kujenga uhusiano kwa mke na mume pindi wanapokwazana husaidia kurejea hali yao ya mwanzo na kudumisha mazingira mazuri zaidi katika maisha ya ndoa pamoja na kupatikana mafanikio mema.

4.3.12 Wanandoa Hubadilika Kimwenendo

Mtafitiwa kutoka katika kijiji cha Chonga alieleza miongoni mwa uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha katika harusi za Wapemba imesaidia kwa kiasi kikubwa kuwabadilisha mke na mume kimwenendo. Jambo hili limetokana na kauli

za nasaha walizopewa kipindi walipoandaliwa kuingia katika ndoa. Mfano mke hunasihiwa ‘asimdai mume kitu ambacho hana uwezo nacho’ na mume huambiwa asimuahidi mke vitu asivyo na uwezo navyo. Kupitia uhusiano wa kauli ya nasaha hii kila mmoja hubadilika. Mke kama alikuwa na tabia ya kupenda mambo makubwa hubadilika na kuwa mtu wa kawaida. Pia kama mume alikuwa na desturi kutoa ahadi kupita uwezo wake hubadilika na kuahidi kile ambacho ana uwezo nacho.

4.3.13 Wanandoa kuwa na Ujasiri

Mtafitiwa kutoka kijiji cha Kipapo alieleza kuwa ndoa ni jambo kubwa ambalo huleta hofu kubwa kwa baadhi ya maharusi. Baadhi ya maharusi wanahisi kama wazazi wao hawana haja nao tena pale wanapopewa waume au wanapohimizwa kuoa. Wengine huona ndoa ni maisha ya utumwa tu kwenda kumtumikia mume. Baada ya wazazi na watu wengine wa familia kukaa nao chini kwa kuwapa kauli za nasaha na kuwaelekeza juu ya umuhimu wa ndoa. Mke na mume wanalainika nyoyo zao kwa kuondokana na woga ambao walikuwa umewajenga katika nafsi zao hapo awali. Kwa hiyo, mume na mke hupata ujasiri wa hali ya juu wa kukabiliana na mchakato wa maisha ya ndoa.

4.3.14 Matayarisho ya Kuingia katika Ndoa

Mtafitiwa kutoka kijiji cha Tondooni Pujini alieleza uhusiano mwengine unaojengwa na kauli za nasaha, huwafanya mke na mume kujiandaa kwa kufanya maandalizi tofauti. Mfano mke hufanya matayarisho ya mapambo ya kila aina kwa ajili ya mume na mume humtayarishia mke mambo mbalimbali kama vile nguo, mapambo, chakula nakadhalika. Pia mume na mke hujitayarisha kwa matayarisho ya usafi wa

mwili na hata wa mazingira ya vitu vilivyomzunguka kuonesha kuwa wanatoka hatua moja na wanakwenda hatua nyengine kubwa ya maisha.

4.3.15 Wanandoa Hufahamu Wajibu Wao

Mtafitiwa katika kijiji cha Limani alieleza kuwa miongoni mwa uhusiano unaojengwa na kauli ya nasaha baina ya mke na mume ni kuelewa kila mmoja wajibu wake kwa mwenzake. Jambo hili hupelekea mke na mume kila mmoja kutekeleza majukumu yake ipasavyo bila ya kuhimizana. Katika jamii ya Wapemba mke hunasihiwa kutekeleza majukumu kama vile, kufanya usafi, kupika, kumshughulikia mume na mengineyo. Mume huhusiwa juu ya wajibu wa kutafuta mahitaji yote ya msingi kwa mke wake kama vile, kutafuta chakula, nguo, malazi, matibabu, kumuelimisha na mengineyo. Pia kila mmoja hujiepusha kutokutekeleza wajibu wake ipasavyo kwa mwenzake. Hii imetokana na kauli za nasaha wanazopewa wakati wanapoingia katika ndoa.

Mtafiti amegundua kuwa katika jamii ya Wapemba kauli za nasaha ambazo hupewa wakati wanapoingaia katika ndoa zimejenga uhusiano kwa mke na mume jambo ambalo limepelekea kuimarika na kudumu katika ndoa zao kadri siku zinavyoendelea katika maisha. Pia kujenga uhusiano mwema baina ya familia moja na nyengine. Kuna baadhi ya watu wanaamini kwamba unapomuoa mwanamke au unapoolewa na mwanamme katika jamii ya Wapemba kuna uwezekano mkubwa wa kudumu ndoa hiyo. Utafiti umegundua kuwa upewaji wa kauli za nasaha wa mara kwa mara katika jamii ya Wapemba ndio msingi imara wa kuzalisha wanandoa wema.

4.4 Muhutasari wa Sura

Sura hii imewasilisha na kuchambua data za utafiti uliofanyika kuhusu kauli za nasaha katika harusi zinavyojenga uhusiano wa wanandoa. Pia sura hii ndio kiini cha utafiti ambapo data iliyopatikana ilichambuliwa pamoja na kupatikana kwa matokeo ya utafiti. Uchambuzi matini ulifanikiwa kufanyika katika lengo la kwanza na la pili na kupatikana kwa matokeo ya utafiti ambayo ndio kilele cha utafiti wenyewe. Hatimaye sura iliyofuata ilihusu muhtasri, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii imekusanya sehemu tano, ambapo sehemu ya kwanza ni utangulizi wa sura. Sehemu ya pili imefafanua muhutasari wa utafiti. Sehemu ya tatu imeelezea matokeo ya utafiti. Sehemu ya nne imetoa hitimisho juu ya utafiti na sehemu ya tano imeelezea mapendekezo ya utafiti.

5.2 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza Kauli za Nasaha katika Harusi Zinavyojenga Uhusiano wa Wanandoa: Mifano kutoka Harusi za Wapemba. Utafiti umefanyika katika Mkoa wa Kusini Pemba ambapo ulishirikisha wilaya mbili ya Mkoani na Chake Chake. Katika wilaya ya Mkoani utafiti ulifanyika katika shehia ya Dodo. Kwa upande wa wilaya ya Chake Chake utafiti ulijumuisha shehia ya Chonga na Matale. Utafiti huu umegawanywa katika sura kuu tano kama ifuatavyo:

Sura ya kwanza, imechambua mambo ya msingi ya utafiti huu. Mwanzo kabisa imeanza na usuli wa mada, tatizo la utafiti, lengo kuu la utafiti, malengo mahsusi pamoja na maswali ya utafiti. Pia imeonesha umuhimu, mipaka ya utafiti pamoja na muhtasari wa sura hiyo.

Sura ya pili, imejumuisha mapitio ya kazi tangulizi, maandiko hayo ni yale yanayohusu kauli za nasaha katika nyimbo za harusi na maandiko ya kauli za nasaha zinazohusu mila na desturi za harusi katika nyimbo za harusi. Pia ndani ya sura hii

kiliainishwa kiunzi cha nadharia ya uchambuzi makini wa matini ambacho kilitumika kuongoza utafiti huu.

Sura ya tatu imehusu mbinu za utafiti. Sura hii imeanza kwa utangulizi mfupi na baadae ikafafanua mkabala wa utafiti, eneo la utafiti, usampulishaji pamoja na kubainisha sampuli ya watafitiwa iliyotumika. Halikadhalika sura hii imechambua mbinu zilizotumika katika ukusanyaji wa data, ambazo ni dodoso, usaili na ushuhudiaji. Mambo mengine yaliyojadiliwa ni vifaa vilivyotumika katika utafiti, kuthibiti na kuaminika kwa data, miiko ya utafiti pamoja na uchambuzi wa data. Mwisho kumalizia na muhtasari wa sura.

Sura ya nne inahusu uwasilishsji na uchambuzi wa data. Sura hii imeanza na utangulizi. Baadae ikafuatiwa na uwasilishaji wa data ambazo zilichambuliwa kwa kufuata malengo mahsusi ya utafiti, ambayo ni kuainisha kauli za nasaha anazopewa biharusi na bwanaharusi kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wapemba na kufafanua uhusiano wa ndoa unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi. Uchambuzi matini ulifanyika, ukiongozwa na nadharia ya uchambuzi makini wa matini. Hatimaye ikamalizia na muhtasari wa sura.

Sura ya tano imetoa muhtasari, hitimisho na mapendekezo. Sura hii imezungumzia vipengele vitano. Kipengele cha kwanza ni utangulizi, kipengele cha pili kimeelezea muhtasari nzima wa utafiti na kipengele cha tatu kimebainisha matokeo ya utafiti. Kipengele cha nne kilitoa hitimisho la utafiti huu na kipengele cha tano kimeonesha mapendekezo ya utafiti.

5.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Baada ya utafiti kukamilika, matokeo ya utafiti yalipatikana kupitia malengo mahsusi mawili ya utafiti kama inavyojionesha hapo chini.

5.3.1 Kuainisha kauli za nasaha anazopewa biharusi na bwanaharusi kwa mujibu wa utamaduni wa jamii ya Wapemba.

Kauli za nasaha katika harusi za Wapemba zimeainishwa katika makundi mawili:

i. Kauli za nasaha za biharusi.
ii. Kauli za nasaha za bwanaharusi

Mfano wa kauli za nasaha anazopewa biharusi:

“Tahadhari sana na ulimi, tunakunasihi, ulimi wako unatakiwa utumie vizuri. Maneno mazuri humtoa nyoka pangoni.”

“Jitahidi sana, kumuomba msamaha mumeo pale unapomkosea, tena urudi matawi ya chini ili upate msamaha wake.”

“Jitahidi sana, mapambo yako yawe kwa ajili ya mumeo tu wala usijipambe ili kujionesha kwa watu wengine.”

Pia mfano wa kauli za nasaha ambazo hupewa bwanaharusi:

“Sikiliza vyema haya tunayokunasihi, mwanamke kaumbwa kwa ubavu uliopinda, ukiamua kuunyoosha unaweza kuukata, ukiamua kustarehe nao, basi starehe nao hali ya kuwa umepinda na ukiamua kuukata basi hiyo ni talaka.”

“Jihadhari sana, usimruhusu mke kuwa na marafiki wengi na kutumia muda mwingi nje kwa kukaa na marafiki zake.”

“Tunakunasihi, haipendezi kwa muumini mwanamme kutengana na muumini mwenzake mwanamke kwa sababu tu amekukera. Wanawake wanapika vyakula

vyetu. Wanafua nguo zetu na wanalea watoto wetu. Inapotokezea mke amekukera, basi isiwe wewe (mume) kushikilia baya alilokutenda ilhali yapo mazuri mengi aliyoyafanya juu yako. Madhali kosa alilokufanyia halivunji heshima ya dini na heshima yako msamehe."

5.3.2 Kufafanua uhusiano wa ndoa unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi.

Kauli za nasaha zimefanikiwa kuonesha uhusiano unaojengwa na kauli hizo kwa bwanaharusi na biharusi katika maisha ya ndoa. Mfano wa uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha kwa bwanaharusi na biharusi:

a) Wanandoa huishi kwa wema.
b) Wanandoa huishi kwa furaha.
c) Wanandoa huishi kwa kuhurumiana.
d) Kushi kwa kushirikiana.
e) Wanandoa hushauriana.
f) Wanandoa huepeuka magomvi.
g) Wanandoa hunasihiana
h) Mume ni kiongozi mke ni mshauri wa familia
i) Mume mtafutaji mke mtunzaji wa mali

5.4 Hitimisho

Utafiti huu kiufupi umeweza kuzikusanya baadhi ya kauli za nasaha tafauti, zilizotolewa katika miktadha ya harusi katika jamii ya Wapemba. Pia tumeweza kuona hali halisi ya utolewaji wa kauli za nasaha hizo pamoja na uhusiano unaojengwa na kauli hizo kwa maharusi katika jamii hiyo. Utafiti umedhihirisha

kuwa kauli za nasaha katika jamii ya Wapemba zimechukua nafasi kubwa katika mila na desturi katika jamii hiyo. Kuna msemo usemao “hoye hoye ndio kilindo” ikimaanisha kwamba bwanaharusi na biharusi wanapopewa kauli za nasaha huwa kama ngao yao na huwaandaa kuwa na maadili bora katika maisha ya ndoa.

5.5 Mapendekezo ya Utafiti

Kauli za nasaha zitolewazo katika harusi zina mchango mkubwa katika kuendeleza maadili mema katika mila na desturi za Wapemba na Waswahili kwa ujumla. Kwa hiyo kauli za nasaha ziendelee kutumika katika jamii hiyo ili kuwajenga wanajamii hao katika kudumisha mwenendo mwema. Pia jamii nyengine hususani jamii za Waswahili zijenge utamaduni wa kupeana kauli za nasaha.

Halkadhalika, mtafiti anapendekeza uchunguzi zaidi ufanyike katika uwanja wa kitaaluma utakaohusisha kauli za nasaha katika miktadha tafauti ikiwemo msibani, maofisini, mashuleni na miktadha mengineo ili kuzijenga jamii kuwa na maadili bora katika sehemu zote wanapokuwepo.

Pia mtafiti anapendekeza watafiti wengine waangalie kauli za nasaha walizopewa wanandoa wakongwe na wanandoa wa sasa halafu walinganishe wepi waliofanikiwa kudumu katika ndoa zao.

MAREJEO

Abdalla, L. (2016). *Athari za itikadi katika nyimbo za harusi za Kizanzibari.* Chuo Kikuu Huria, Tanzania.

Ameir, H. (2007). *Maadili yanayopatikana katika nyimbo za ukungwi wa Zanzibari*. Chuo Kikuu chaTaifa cha Zanzibar, (Haijachapishwa).

BAKITA, (2017). *Kamusi kuu ya Kiswahili*. Longhorn: Nairobi, Kenya.

BAKIZA, (2010*). Kamusi la Kiswahili fasaha*. Oxford University Press: Kenya.

Coppens, F. (1980). *Wedding customs in Lamu society*. Longhorn: Nairobi, Kenya.

Enon, C. J. (1998). *Education research and measurement, department of distance education*. Makerere University: Uganda.

Fairclough, N. (1995b). *Critical discourse analysis*. London: Longman.

Farsy, M. S. (1967). *Ada za harusi katika Unguja*. Kenya Literature Bureau, Nairobi.

Gora, S. H. (2015). *Utani katika sherehe za harusi za Watumbatu: Aina, sababu na taashira zake.* Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania.

Harries, L. (1965). *Swahili prose text.* Oxford University Press, Nairobi**.**

Hymes, D. (1964). *Foundations in social linguistics*. Philadelpia University of Pennyslavania.

https://www.jamiiforums.com. Imepakuliwa tarehe 15/9/2021.

Kavugha, F. S. (1997). *Desturi na mila za Wapare*. Vuga Press Soni, Kenya.

Kothari C. R. (2009). *Research methodology: Methods and techniques.* New Delhi: Wiley Easten, Wishwa Prakashan.

Mazigwa, S.A. (1991). *Fasihi ya Kiswahili,* Ndanda-Peramiho, Benedictine Publication.

Mohamed, A. M. & Mohamed, S. A. (1998). *Kamusi ya visawe*, East African Educational Publisher: Nairobi.

Muhammed, O. S. (2010). *Mchango wa nyimbo za unyago katika kumuandaa mwari na maisha ya unyumba.* Chuo Kikuu cha Kiislamu Uganda.

Muhammed, S. (2007). *Athari ya nyimbo za harusi kwa mke na mume, Zanzibar.* Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Ngure, A. (2003). *Fasihi simulizi kwa shule za sekondari*. Phoenix Nairobi.

Nkwera, F. R. (1998). *Tamrini za fasihi simulizi sekondari na vyuo*. Business Printers Limited, Dar es Salaam.

Said, M. M. (2012*). Uchanganuzi wa maadili ya unyumba katika nyimbo za harusi.* Chuo Kikuu cha Kiislamu, Uganda. (Haijachapishwa).

Schiffrin, D. (1984). *Meaning, form and use in context: Linguistic applications*. Washington DC Georgetown university Press.

Suleiman, K. A. (2015). *Kuchunguza kiwango cha mabadiliko ya matumizi ya msamiati wa Kipemba.* Chuo Kikuu Huria, Tanzania.

Timammy, R. (2002). *Swahili women's wedding songs; A stylistic analysis*. Nairobi: University. Kenya.

TUKI, (1981). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press, Kenya.

TUKI, (2004). *Kamusi ya Kiswahili sanifu.* Oxford University Press, Kenya.

TUKI, (2010). *Kamusi ya Kiswahili sanifu*. Oxford University Press, Kenya.

Widdowson, H. G. (1995). *Discourse analysis: a critical view*. Lang. Lit 4 (3): 157 – 72, International journal of staylestics. Georgetown University Press, Washington D.C.

VIAMBATANISHO

Kiambatanisho A: Maswali ya usaili kwa wanandoa wakongwe

Tafadhali naomba usaidie kujibu maswali haya kwa mujibu unavyoyaelewa ili kusaidia kupata data za uhakika zitakazo kamilisha utafiti huu.

1. Unafahamu nini kuhusu kauli za nasaha
2. Kuna miktadha mingapi itolewayo kauli za nasaha katika harusi za Wapemba?
3. Ainisha miktadha (mazingira au maeneo) ambayo kauli za nasaha hutolewa katika harusi za Wapemba?
4. Taja kauli za nasaha zinazopatikana kwa kila muktadha.
5. Taja lengo la kauli za nasaha hizo.
6. Ni yupi kati ya harusi wa kike na wa kiume anaepewa kauli za nasaha zaidi?
7. Eleza sababu ya jibu lako?
8. Je, kauli za nasaha zinajenga uhusiano kwa maharusi?
9. Elezea uhusiano huo unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi.
10. Kwa maoni yako, kama kauli za nasaha zisingalitumika je, ndoa zisingalidumu?

Ahsante Sana kwa Mashirikiano Mema

Kiambatanisho B: Mwongozo wa maswali ya usaili kwa mashekhe

Tafadhali naomba usaidie kujibu maswali haya kwa mujibu unavyoyaelewa ili kusaidia kupata data za uhakika zitakazo kamilisha utafiti huu.

1. Kwa uelewa wako unafahamu nini kuhusu kauli za nasaha?
2. Je, kuna kauli za nasaha zozote ambazo huwa unawapatia maharusi?
3. Ni wakati gani ambapo huwapa maharusi kauli za nasaha hizo?
4. Unaweza kunisaidia kwa kunielezea kauli za nasaha ambazo unawapa maharusi?
5. Je, kauli za nasaha zina uhusiano kwa bwanaharusi na biharusi?
6. Fafanua uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi?

Ahsante Sana kwa Mashirikiano Mema

Kiambatanisho C: Mwongozo wa maswali ya dodoso kwa wanandoa wapya

Tafadhali naomba usaidie kujibu maswali haya kwa mujibu unavyoyaelewa ili kusaidia kupata data za uhakika zitakazo kamilisha utafiti huu.

1. Unafahamu nini kuhusu kauli za nasaha

……
……
……..

2. Je, ulipewa kauli za nasaha wakati wa kuingia katika ndoa? ……

3. Taja maeneo ambayo ulipewa kauli za nasaha kuhusu ndoa yako.

1. ……
2. …….....
3. ……
4. ……..
5. ……..
6. …….

4. Taja kauli za nasaha ulizopewa kwa kila eneo.

1. ……
2. ……
3. ……
4. ……
5. ……
6. ……

5. Je, kauli za nasaha zinajenga uhusiano kwa bwanaharusi na biharusi?
……..…….

6. Taja uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha kwa maharusi

1. ……..
2. ……..
3. ……..
4. …….
5. …….
6. …….

Ahsante Sana kwa Mashirikiano Mema

Kiambatanisho D: Mwongozo wa maswali ya usaili kwa makungwi

Tafadhali naomba usaidie kujibu maswali haya kwa mujibu wa uelewa wako ili kusaidia kupata data za uhakika zitakazo kamilisha utafiti huu.

1. Kwa uelewa wako unadhani ni nini kauli za nasaha?
2. Je, kuna kauli za nasaha ambazo unawapa bwanaharusi na biharusi wakati unapowapeleka katika makaazi yao?
3. Unaweza ukanipatia kauli za nasaha hizo.
4. Je, kauli za nasaha unazowapa zinajenga uhusiano kwa bwanaharusi na biharusi?
5. Elezea kauli za nasaha ambazo zinajenga uhusiano kati ya bwanaharusi na biharusi.

Ahsante Sana kwa Mashirikiano Mema

Kiambatanisho E: Mwongozo wa maswali ya usaili kwa walimu wa kike wa madrasa

Tafadhali naomba unisaidie kujibu maswali haya kwa mujibu unavyoyaelewa ili kusaidia kupata data za uhakikka zitakazokamilisha utafiti huu.

1. Unafahamu nini kuhusu kauli za nasaha?
2. Je, zipo kauli za nasaha ambazo huwapa maharusi?
3. Unaweza kunielezea kauli za nasaha hizo?
4. Elezea kauli za nasaha unazowapa maharusi?
5. Je, kauli za nasaha hizi zinajenga uhusiano kwa maharusi?
6. Elezea uhusiano unaojengwa na kauli za nasaha?

Ahsante Sana kwa Mashirikiano Mema

Kiambatanisho F: Ratiba na mchakato wa utafiti

TAREHE	TUKIO
22/06/2021	Uwasilishaji wa Pendekezo la Utafiti
26/06/2021 – 08/07/2021	Marekebisho ya Pendekezo la Utafiti
16/07/2021 – 25/07/2021	Kufanya marekebisho ya mwisho ya pendekezo la utafiti
04/08/2021	Kupriniti pendekezo la utafiti
08/08/2021 – 16/08/2021	Ukusanyaji wa data
17/08/2021 – 26/08/2021	Uchambuzi wa data
02/09/2021 – 10/10/2021	Kuandika ripoti ya utafiti
16/10/2021 – 26/10/2021	Marekebisho ya ripoti ya Utafiti
15/11/2021	Uwasilishaji wa ripoti ya Utafiti
23/11/2021- 30/11/2021	Marekebisho ya ripoti ya Utafiti
05/12/2021- 10/12/2021	Uchapishaji wa vitabu vya tasnifu
25/12/2021	Kukabidhi vitabu vya tasnifu

Kiambatanisho G: Bajeti

Sehemu hii inahusisha makisio ya fedha yaliyotumika ili kukamilisha utafiti huu. Makadirio hayo yalihusisha matumizi ya fedha kuanzia mwanzo wa uandishi wa pendekezo la utafiti mpaka mwisho wa kukamilika kwa ripoti ya utafiti ambapo uliambatana na shughuli mbalimbali kama ukusanyaji wa data, kuzichambua, kuandika ripoti ya utafiti pamoja na nauli za safari kwa ajili ya kukamilisha uandishi wa utafiti. Chanzo cha upatikanaji wa fedha hizo ni nguvu zake mtafiti binafsi.

	VIFAA	**IDADI**	**MAKADIRIO**	**JUMLA**
01	Karatasi	Rimu 10	10 x 10000	100,000/=
02	Madaftari ya kuhifadhia data	4	1 x 5000	20,000/=
03	Kalamu	Boksi 1	1 x 15000	15,000/=
04	Flash	01	1 x 40000	40,000/=
05	Kompyuta	01	1 x 750,0000	750, 0000/=
			JUMLA	**925,000/=**
	MATUMIZI MENGINE			
06	Chakula	Miezi 5	1x 7000	1,050,000/=
07	Usafiri	Miezi 5		1,000,000/=
08	Mawasiliano	Miezi 5		100,000/=
			JUMLA	2,150,000/=
			JUMLA KUU	**3,075,000/=**

Kiambatanisho H: Kibali cha utafiti

REVOLUTIONARY GOVERNMENT OF ZANZIBAR

SECRETARY
ZANZIBAR RESEARCH COMMITTEE
P. O Box 239
Tel: 2230806
FAX: 2233788

RESEARCH/FILMING PERMIT
(This Permit is only Applicable in Zanzibar for a duration specified)

P.O. Box 2321

SECTION

Name:	Fatma Yakout Biroli
Sex	Female
Date and Place of Birth	06/03/1981
Nationality:	Tanzanian
Passport Number:	-
Date and Place of Issue	-
Date of arrival in Zanzibar	-
Expected date of departure	-
Duration of study	One Year
Research Tittles	Matumizi ya Lugha ya Nasaha katika Muktadha wa Harusi za Kipemba: Mfano kutoka Mkoa wa Kusini Pemba
Full address of Sponsor	
Name of the authorizing officer:	Abdalla M. Denge
Signature and seal:	
Institution:	Office of Chief Government Statistician
Address:	P. O Box 2321 Zanzibar.
Date:	**07/09/2020**

S. M. Z
P.O. Box 2321

Kiambatanisho I: Ruhusa ya kufanya utafiti

SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

P. O. Box 239
Vuga Street
Zanzibar-Tanzania

Tel. 024 22 30808
Fax. 024 22 30808
E-mail : ps 2vpo@zanzibar.go.tz

OMPR/M.95/C.6/2/VOL.IX/ 17/09/2020

MHESHIMIWA,
MKUU WA WILAYA,
WILAYA YA CHAKECHAKE,
PEMBA.

MHESHIMIWA,
MKUU WA WILAYA,
WILAYA YA MKOANI,
PEMBA.

KUH: RUHUSA YA KUFANYA UTAFITI

Kwa heshima, naomba uhusike na mada ya hapo juu.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imemruhusu **Ndg. Fatma Yakout Biroli** mtafiti Mwanafunzi kutoka **Chuo Kikuu cha Zanzibar** ambae anasomea **Shahada ya Uzamili** katika fani ya **Sanaa ya Kiswahili** kufanya utafiti katika mada inayohusiana na "Kauli za Nasaha zinavyojenga uhusiano wa wanandoa: Mifano kutoka Harusi za Wapemba" Utafiti huo utafanyika katikaWilaya yako kuanzia tarehe **17/09/2020** mpaka **17/09/2021.** Tunaomba asaidiwe ili aweze kukamilisha utafiti huo.

Kwa nakala ya barua hii mara baada ya kumaliza utafiti, mtafiti unatakiwa kuwasilisha nakala (copy) 3 za ripoti ya utafiti huo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais- Zanzibar.

Naambambatanisha na kivuli cha kibali cha kufanyia utafiti.

Wako mtiifu,

Khalid Bakari Hamran

KHALID B. HAMRANI,
/KATIBU MKUU,
OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS,
ZANZIBAR.

NAKALA: Ndg. Fatma Yakout Biroli.